# Nipashe

Jumamosi Desemba 14, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580101

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

ARIGATOU INTERNATIONAL GNRC CEFA




## Magereza yaanika sababu za wafungwa wa msamaha kuiba

UK. 3

# Membe, Kinana, Makamba kuwekwa kikaangoni CCM

**January,** Nape, Ngeleja roho kwatu... Dk. Batilda, Kamanda Zelothe kuchuana uenyekiti Arusha... *Uk 2*



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa tatu kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mpango wa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha uliofanyika jana, Jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**UPENDELEO MIRADI WAMCHEFUA DC**
MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amefanikiwa kupata Sh. milioni 338 ili kujenga kituo cha afya huku akikemea.

UKURASA WA 2

**JPM KUONGOZA MAPOKEZI NDEGE**
RAIS John Magufuli leo anatarajiwa kuongoza mapokezi ya ndege ya serikali iliyokuwa inashikiliwa Canada...

UKURASA WA 7

**200 WAFIKISHWA MIREMBE KILA SIKU**
ASILIMIA 75 ya wagonjwa wa afya ya akili wanaofikishwa Mirembe ni wanaume huku hospitali ikipokea wagonjwa 200 hadi 300 kila siku

## MDEE ATETEA NAFASI CHADEMA

UK.3

# Daktari kortini tuhuma kuomba rushwa ya ngono

UK. 2

**MICHEZO** SVEN AISHIKA SIMBA MSHIPA WA FAHAMU UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

## JPM kuongoza mapokezi ndege iliyokamatwa leo

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

RAIS John Magufuli leo anatarajiwa kuongoza wananchi mkoani Mwanza kupokea ndege aina ya Bombardier Q400 iliyokuwa imekamatwa Canada.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema ndege hiyo itapokewa katika jengo jipya la Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Alisema Rais Magufuli ataongoza wananchi watakaojitokeza katika mapokezi ya ndege hiyo.

'Ile ndege yetu iliyokuwa imekamatwa kule Canada, sasa imeachiwa. Kwa furaha sana, kwa niaba ya wana Mwanza kesho (leo), Mheshimiwa Rais pale uwanja wa ndege jengo jipya, atatuongoza kupokea ndege yetu, ambayo imenunuliwa kwa fedha za Watanzania.

"Nimekuja hapa kuwatangazia wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi, kuanzia saa nane kamili geti litakuwa wazi, hata kabla ya hapo mpaka saa 10 atakapokuja Rais, tujitokeze kwa wingi kuunga mkono juhudi za Rais," aliomba. Novemba 23, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akiwa Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma, alitangaza kushikiliwa kwa ndege hiyo Canada. Prof. Kabudi alidai kumekuwa na hujuma kubwa zinazofanywa na mabeberu kwa lengo la kurudisha nyuma juhudi na maendeleo ya nchi.

Alisema mara baada ya ndege hiyo kukamatwa, alimwita Balozi wa Canada nchini na kumweleza namna Serikali ya Tanzania inavyokasirishwa na vitendo vya ndege zake kukamatwa nchini humo kila ikifikia hatua ya kurudi Tanzania.

"Limetokea jambo la kusikitisha ambalo ni vyema Watanzania pia walielewe jinsi ambavyo hujuma za kibeberu zinafanyika kurudisha kasi ya maendeleo, tena kwa mara ya tatu ndege ambayo ilitakiwa kufika Tanzania, imekamatwa tena Canada na kesi ipo mahakamani.

"Aliyefanya hivyo ni mtu yuleyule aliyekamata ndege yetu Afrika Kusini, tukaenda mahakamani tukamshinda, sasa amekimbilia Canada na amekamata ndege yetu ya Bombadier Q400," alisema.

# Membe, Kinana, Makamba kikaangoni

**Na Romana Mallya**

HALMASHAURI Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeazimia wanachama wake watatu, Abdulrahman Kinana, Yusuf Makamba na Bernard Membe, waitwe na Kamati ya Usalama na Maadili ili wajibu tuhuma za kimaadili zinazowakabili.

Wakati vigogo hao wakiwekwa kikaangoni, NEC imewasamehe na kutoa tahadhari kwa Mbunge wa Bumbuli, January Makamba, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye na Mbunge wa Sengerema, William Ngeleja.

Maazimio hayo yametokana na kikao chake kilichofanyika jana jijini Mwanza chini ya Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, NEC imeamua Mzee Makamba, Membe na Kinana waitwe na kuhojiwa na kamati hiyo kujibu tuhuma zao kwa mujibu wa Katiba ya Chama na Kanuni za Maadili na Uongozi.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa kikao hicho kilipokea, kujadili na kuridhia kwa kauli moja taarifa ya Kamati Kuu kuhusu uamuzi wa Mwenyekiti wa CCM wa kuwasamehe wanachama walioomba radhi kwake.

"Walioomba radhi kwake ni January Makamba, Nape na Ngeleja baada ya kukiri mbele yake kufanya makosa ya kimaadili yaliyokidhalilisha chama na viongozi wake mbele ya umma," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, kikao hicho kimewataka wanachama hao kujirekebisha na kutorudia makosa yao la sivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na taratibu za chama ikiwamo kufukuzwa uanachama.

**WATEULIWA KUGOMBEA**

Taarifa hiyo ilisema awali Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM imefanya uteuzi wa majina ya wagombea wa nafasi za uongozi katika chama na jumuia.

"Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha ni Dk. Batilda Buriani, Zelothe Stephen na Bakari Msangi. Wagombea wa nafasi ya Katibu wa Siasa na Uenezi Mkoa wa Iringa ni Mafanikio Kinemelo, Hilary Kipingi na Lucas Lwimbo,"ilitaja.

Kwa upande wa wagombea wa nafasi ya Katibu wa Siasa na Uenezi Mkoa wa Mtwara, taarifa hiyo iliwataja waliopitishwa kuwa ni Petro Mwendo, Mustafa Mohamed na Selemani Sankwa na wakati wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Dodoma ni Damas Kasheegu, Baraka Mkunda na Christopher Mullemwah.

"Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Pwani ni Mary Joseph, Fredrick Makachila na Samaha Said," ilieleza taarifa hiyo.

**MSIMAMO WA JPM**

Katika kikao hicho, taarifa ilieleza kuwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Magufuli, amesisitiza kazi ya urais ni ngumu na ataheshimu utamaduni na desturi za CCM, Kanuni, Katiba ya CCM na Katiba ya nchi.

Rais Magufuli, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alisema CCM ni kiwanda cha kuzalisha viongozi na kwa utaratibu ambao chama kimejiwekea kitampata mtu bora zaidi atakayepokea uongozi baada yake.

"Nawashukuru sana viongozi wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama chetu kwa kuzisimamia vizuri serikali zetu mbili, hivyo kuwezesha kupatikana mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya CCM.

"Tukaendelee kujenga umoja, kuimarisha ujenzi wa chama na tunapoelekea katika chaguzi zinazokuja tukaepuke makundi na tuendelee kuisimamia serikali ikiwamo kukagua miradi ya kimaendeleo katika maeneo yetu," alisema Rais Magufuli.




Wafanyausafi wakitoa mchanga pembeni ya barabara huku wakiwa hawajaweka alama ya tahadhari hali inayoweza kuhatarisha maisha yao katika eneo la Kwa Warioba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Daktari kizimbani tuhuma kuomba rushwa ya ngono

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

DAKTARI Massoud Suleiman Abdallah, amependishwa kizimbani katika Mahakama ya Chake Chake, Pemba, akikabiliwa na mashtaka ya kumuomba rushwa ya ngono mgonjwa.

Daktari huyo anatuhumiwa kuomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa ambaye ni mama mjauzito aliyefika Hospitali ya Chake Chake kwa ajili ya matibabu.

Baada ya mtuhumiwa huyo kupanda kizimbani, alisomewa shitaka lake na mwendesha mashitaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ramadhan Suleiman Ramadhan.

Mwendesha Mashtaka huyo alidai mtuhumiwa alitenda makosa mawili, la kwanza likiwa la Novemba 21, mwaka huu majira ya kati ya saa 3:55 na saa 4:00 asubuhi, katika Hospitali ya Chake Chake, aliomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa aliyekwenda hospitalini hapo kwa ajili huduma ya uchunguzi ya ultra sound.

Alidai kitendo hicho ni kosa kisheria kwa kuwa ni kinyume cha Kifungu cha 58 cha Sheria ya Rushwa Na. 1 ya Mwaka 2019 ya sheria za Zanzibar.

Alidai kosa la pili lilifanyika siku hiyo hiyo, kwamba mtuhumiwa akiwa mwajiriwa wa serikali katika Wizara ya Afya, alitumia nafasi yake vibaya kwa kutaka kufanya ngono na mgonjwa aliyefika hospitali kwa ajili ya matibabu.

Alidai kufanya hivyo ni kosa kisheria kwa kuwa ni kinyume cha Kifungu cha 53 na 61 cha Sheria Na. 1 ya Mwaka 2012 ya sheria za Zanzibar.

Mshtakiwa alikana kutenda makosa hayo na kuiomba mahakama impatie dhamana kupitia mawakili wake, ombi ambalo lilikubaliwa na mahakama kwa masharti ya wadhamini wawili ambao ni wafanyakazi wa serikali na kutia saini bondi ya Sh. milioni mbili.

Mshitakiwa alitimiza masharti na kesi hiyo itatajwa tena mahakamani huko Febuari 27, mwakani. Novemba 21, mwaka huu, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (Zaeca) kisiwani Pemba, ilimkamata daktari huyo akituhumiwa kuomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa wake kama malipo ya huduma ya uchunguzi ya ultra sound.

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, akizungumza jijini Dar es Salaam jana na wakufunzi kutoka vyuo mbalimbali walioshiriki kozi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto (ECD) kwa watoto chini ya miaka mitano kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC). Kulia ni Mkurungezi wa Karibu Tanzania Organization ('KTO), Majidi Mjengwa na kushoto Mkurugenzi wa Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, Dk. Noel Mbonde. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bosi Magereza aanika sababu za wafungwa waliosamehewa kuiba

**Na Romana Mallya**

JESHI la Magereza limeeleza kinachosababisha wafungwa wanaoachiwa kwa msamaha wa Rais, kurudia makosa kwamba, ni jamii kutowapokea kama watu waliobadilika kitabia na wenye ujuzi waliofundishwa gerezani.

Vilevile, limesema jambo lingine linalowasukuma watu hao kurudia kutenda makosa ya uhalifu ni hofu na shaka anayokuwa nayo mfungwa anaporudi kwenye jamii aliyoikosea awali.

Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike, alitaja sababu hizo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu wafungwa 5,533 walioachiwa Jumanne kwa msamaha wa Rais John Magufuli huku baadhi yao wakirudia makosa muda mfupi baada ya kufika uraiani.

Kamishna Jenerali Kasike alisema kitendo cha wafungwa kurudia makosa pindi wanapoachiwa, kinasababishwa na jamii kutowapokea kama watu waliobadilika.

"Tunapokuwa na wafungwa magerezani, tunafanya urekebishaji wa aina mbili: Kwanza, tunawapa ushauri nasaha kuwaonyesha kuwa walichokitenda hadi kuingia magereza ni kosa.

"Pili, tunawapa mafunzo, wanajifunza mambo mbalimbali pamoja na stadi za kazi ili wakitoka wawe na ujuzi na wanapata mafundisho ya kiroho kila mara kupitia watumishi wa Mungu wanaokwenda magerezani," alisema.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Magereza alisema jukumu la urekebishaji wa tabia za mwanadamu ni suala mtambuka na endelevu linalohusisha jeshi hilo na jamii.

"Jamii iwe tayari kuwapokea wafungwa waliopata msamaha, watambue wamejutia makosa yao na wamejirekebisha, wawape msaada kwa sababu katika jamii wanaweza kukaa nao ili wabadilike taratibu.

"Jamii iwapokee ili wajione nao ni sehemu ya jamii, kwa kufanya hivyo, tutasaidia kuwawezesha kurudi katika maisha ya awali yanayozingatia sheria na taratibu za nchi, tuache kuwanyanyapaa, unyanyapaa utawaathiri na kusababisha warudi kwenye makosa.

"Tatizo tulilonayo ni baadhi ya wafungwa kuonyesha kuwa hawako tayari kungana na jamii, hivyo kurejea kutenda makosa mara baada ya kuachiwa huru. Ila tumekamilisha kazi hii ya kuwaachia huru wafungwa waliopata msamaha wa Rais," alifafanua.

Kuhusu mfungwa aliyetoka na mtoto, alisema zipo taratibu za magereza ambapo kabla hawajaingia magerezani hupimwa afya zao ikiwamo ujauzito.

"Wakishapimwa hususani wanawake, tunajua kwamba ameingia na ujauzito, kwa hao wanaotoka na watoto ndivyo ilivyo, yawezekana alipoingia alikuwa na ujawazito, akajifungulia gerezani," alisema.

Kamishna Jenerali Kasike alibainisha kuwa magereza yote nchini yana uwezo wa kuchukua watu 29,902 na kwamba kabla ya msamaha, walikuwa na wafungwa 17,805 na kwa sasa waliobaki ni 12,665.

"Ili mfungwa au mahabusi akae gerezani lazima awe na hati ya mfungwa au mashauri ndipo anapokelewa gerezani kinyume chake hawezi kupokelewa, yule aliyekataa kwa mujibu wa taratibu siyo mfungwa tena, kesi ilishafutwa, tuliwasiliana na ndugu zake wakamchukua," alisema.

Pia, alisema mfungwa anapoachiwa, hupewa nauli kumtoa pale alipomaliza kifungo chake kumrejesha alipofungwa.

Kamishna Jenerali Kasike alitaja manufaa ya msamaha kwa wafungwa kuwa yanapunguza msongamano, wanufaika kujumuika na ndugu zao na kujishughulisha na shughuli za maendeleo.

"Msamaha ni kichocheo cha urekebishaji magerezani, kuimarisha nidhamu na kurejesha matumaini kwa wanaobaki," alisema.

Alisema msamaha hutolewa kwa kuzingatia uzito wa baadhi ya makosa na kwamba hauhusishi wafungwa wa kunyongwa, waliofungwa maisha, kesi za dawa ya kulevya, rushwa na wizi wa kutumia silaha.

"Msamaha haujahusisha wizi wa nguvu, makosa ya kujamiiana, kulawiti, kuwapa mimba wanafunzi, kubaka, wizi wa magari, uharibifu wa miundombinu, walionufaika na parole na uhujumu uchumi," alisema.

# Mdee atetea kiti Chadema

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Kawe, Halima Mdee, amefanikiwa kutetea nafasi ya uenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bawacha) katika uchaguzi uliofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Mdee ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, ametetea nafasi hiyo kwa kupata kura 312 za ndiyo dhidi ya saba za hapana. Akitangaza matokeo hayo, msimamizi wa uchaguzi huo, Slyvester Masinde, alisema Mdee kuwa mwenyekiti wa Bawacha huku Hawa Mwaifunga akitangazwa kuwa makamu mwenyekiti wa baraza hilo baada ya kupata kura 220 na kuwabwaga wapinzani wake watatu.

Katika uchaguzi huo, Mdee anayeingia kipindi cha pili cha uongozi wa baraza hilo, hakupata mpinzani katika nafasi yake sawa na ilivyokuwa kwa katibu wa baraza hilo na Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, akipata kura 35 za ndiyo na moja ya hapana. Kwenye nafasi ya makamu mwenyekiti, mbali na Mwaifunga aliyeibuka mshindi, wagombea wengine ni Aisha Luja ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kati aliyepata kura 68, Mary Nyagabona kura 26 na Stella Chozaile kura 14.

Uchaguzi wa viongozi ndani ya chama hicho unatarajiwa kukamilika Desemba 18, mwaka huu kwa kumchagua mwenyekiti wa chama hicho.

Mpaka sasa, walioijitokeza kuwania nafasi hiyo ni Mbunge wa Hai, Freeman Mbowe na Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe.

Waziri Mkuu mstaafu Frederick Sumaye pia alikuwa amejitosa kuwania nafasi hiyo, lakini alijiengua wiki iliyopita baada ya kutangaza kujivua uanachama wa Chadema kutokana na kile alichodai 'hakuna demokrasia'.



# Upendeleo wa miradi wamchefua mkuu wilaya

**Na Godfrey Mushi,** HAI

UPENDELEO wa uwekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika ukanda wa milimani wilayani Hai, umemchefua Mkuu wa wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya na kuagiza kuanzia sasa huduma kama afya, barabara na elimu kuelekezwa ukanda wa chini wa tambarare.

Ole Sabaya aliagiza jana kumalizwa kwa malalamiko hayo ya wananchi wa tambarare, alipozindua ujenzi wa Kituo cha Afya cha Heshima cha Longoi kinachojengwa katika Kata ya Weruweru.

"Nimesikia malalamiko yenu kwamba kila mradi ukija unaelekezwa ukanda wa milimani (Machame na Masama) na nyie hata barabara hazipitiki.

"Najua kuna kinamama wajawazito wanateseka kupita lile daraja la Mnepo kuja Kwa Sadala hadi Hospitali ya Wilaya. Mkurugenzi Mtendaji (Yohana Sintoo) naomba tatizo hili ulimalize na yasijitokeze tena malalamiko haya, ndiyo maana leo (jana) tumewaletea kituo hiki cha afya cha heshima kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais John Magufuli," alisema.

Kituo hicho kitahudumia zaidi ya wananchi 19,000 wa kata tatu za Weruweru, Masama Rundugai na Mnadani.

Kwa miaka 58, sasa wananchi hao wamekosa huduma za afya na kulazimika kuzifuata umbali wa zaidi ya kilomita 20.

"Maeneo haya ya tambarare yamekuwa yakionekana kama yametengwa na kubaguliwa huku maeneo ya juu milimani yakionekana kuwa na maendeleo ikiwamo kuwa na huduma zote muhimu za kijamii.

"Baada ya kuona dhana hiyo iliyojengeka kwenu, nilibuni namna ya kuwasaidia kwa kufanya jitihada za kutafuta fedha ili kujengwa kwa kituo hiki ambacho kinatarajiwa kuhudumia maelfu ya wananchi wa maeneo haya ya tambarare," alisema.

Akizungumza wakati akizindua ujenzi huo, Ole Sabaya alisema kituo hicho kitagharimu zaidi ya Sh. milioni 300, fedha ambazo zinatokana na michango kutoka katika vyama vya ushirika.

"Fedha hizi zimetolewa na vyama vya ushirika, tuliwaomba katika bajeti yao ya mwaka 2018/2019 kutenga asilimia 50 kwa ajili ya kuchangia ujenzi huu, lakini pia pamoja na hilo bado wananchi mnapaswa

INAENDELEA UK. 8

# Waziri aagiza mhandisi akamatwe

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ameliagiza Jeshi la Polisi kumkamata na kumsweka ndani Alistides Kanyomo, mhandisi wa Kampuni ya Mbesso Construction Ltd ya jijini Dar es Salaam, kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni tatu za mradi wa maji katika Bonde la Mwakaleli wilayani Rungwe.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea mradi huo ulioanza miaka 11 iliyopita, lakini mpaka sasa haujakamilika na hivyo kusababisha wananchi katika vijiji 18 vya Halmashauri za Busokelo na Rungwe kukosa huduma ya maji.

Alisema baada ya kupitia mpango kazi wa mradi huo, amebaini ubadhirifu mkubwa wa fedha za mradi, hali ambayo alidai serikali haiwezi kuvumilia. Waziri huyo alisema katika mpango kazi huo, ameona andiko linaloonyesha kuwa ofisi ya muda ya kampuni hiyo iliyojengwa kwenye eneo la mradi imegharimu Sh. milioni 100, lakini alipofika kuikagua, akabaini ni kibanda kidogo cha mabati ambacho hakiwezi kugharimu hata Sh. milioni moja.

"Wamelipwa Sh. bilioni tatu mpaka hivi sasa, lakini hakuna ambacho kimeshafanyika, hapa ninaona kuna kibanda wamejenga kwamba ni ofisi zao za muda, wanadai wamekijenga kwa Sh. milioni 100 wakati ni cha mabati kuanzia chini mpaka juu," alilalama.

Alisema serikali haiwezi kuvumilia fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi zikichezewa kwa kiwango hicho, hivyo akaagiza askari polisi kumkamata msimamizi wa mradi huo, Kanyomo na kumweka ndani ili kupisha uchunguzi wa matumizi ya fedha hizo.

"Naagiza mkamateni mhandisi anayesimamia mradi huu bila kujali kama ndiye mmiliki wa kampuni au la, mwekeni ndani ili tuchunguze kwanza matumizi ya fedha zilizotumika kama zinaendana na kazi iliyofanyika," aliagiza.

Prof. Mbarawa pia aliiagiza Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA) kuvunja mkataba na mkandarasi huyo mara moja ili mradi huo usimamiwe moja kwa moja na serikali kupitia mamlaka hiyo ili kuhakikisha mradi huo unakamilika na wananchi hao wanapata maji haraka.


Awali, Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, alidai wananchi wa Mwakaleli wanapata shida ya upatikanaji wa maji, hivyo akaiomba serikali kusimamia yenyewe mradi huo ili kuhakikisha wananchi hao wanapata maji.

Alisema mradi huo umechukua muda mrefu kiasi kwamba wananchi wameanza kupoteza imani na serikali kutokana na kukosa huduma ya maji.

"Mradi huu ulianza tangu mwaka 2008 na sasa ni mwaka 2019, umechukua miaka 11 bila kukamilika, wananchi wetu wameanza kukata tamaa, hivyo nakuomba waziri uwaondoe hawa makandarasi na badala yake mradi huu usimamiwe moja kwa moja na serikali ili wananchi wangu wapate maji," aliomba.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema alipoingia wilayani Rungwe mwaka 2016, alikuta miradi miwili ya Masoko na Mwakaleli ikiwa na matatizo makubwa na kwa kushirikiana na Wizara ya Maji waliamua kuanza kushughulikia mradi mmoja mmoja ili kumaliza matatizo yaliyokuwapo.

Alisema walianza na mradi wa Masoko ambao kwa sasa unaendelea vizuri na sasa wameamua kugeukia mradi huo wa Mwakaleli ili kutatua matatizo yake na kuhakikisha wananchi wa eneo hilo wanapata maji safi na salama.




Meneja wa Kampuni ya Mawasiliano Tigo, Kanda ya Kusini, Abass AbdulRahman (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh Milioni tano Desteria Mallole wa mjini Iringa baada ya kuibuka mmoja kati ya washindi nane wa wiki wa Kampeni ya Kishindo cha Funga Mwaka

# Waziri awaonya mafisadi bandari

**Na Elizabeth Zaya,** BUKOBA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isaack Kamwelwe, amesema uendeshaji wa bandari nchini hautarudishwa nyuma tena kama ilivyokuwa imefanywa na mafisadi.

Kamwelwe alitoa kauli hiyo jana alipotembelea Bandari za Bukoba na Kemondo zilizoko mkoani Kagera.

Alisema baada ya bandari nyingi kusitisha shughuli zake kwa kipindi kirefu kulikosababishwa na matatizo mbalimbali, wakiwamo mafisadi waliokuwa wakipenda kujinufaisha wenyewe, serikali imeanza mkakati wa kuzifufua na kuboresha zaidi zinazofanya kazi.

"Tunafanya maboresho katika bandari zetu zote, tunataka turudishe huduma kwa kasi kubwa hata kwa zile ambazo zilikuwa zimesitisha huduma zake, ulifanyika uzembe, waliturudisha nyuma mafisadi, lakini tumefanikiwa kunyanyuka, hatutakubali kurudishwa nyuma tena walikokuwa wametufikisha.

"Juhudi zinazofanywa na Rais John Magufuli za kukarabati bandari na meli, meli zinabadilika zinakuwa mpya, hususani meli ya Mv Victoria na Mv Butiama ambazo mpaka Aprili mwakani zitaanza kufanya kazi.

"Nimekuja kukagua maboresho haya yanayofanyika, kazi inaendelea vizuri na ninaipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa kazi kubwa wanayofanya katika uboreshaji huu wa bandari.

"Usafiri wetu wa raha uliopotea kwa miaka mingi, sasa unarudi, Mv Victoria sasa itatoa huduma zake katika ziwa hili na itafika Uganda mpaka Kenya, tunatarajia wananchi wataondokana na shida ya usafiri ambayo imekuwapo kwa muda mrefu," alisema.

Akizungumzia maboresho yanayofanyika katika reli, Kamwelwe alisema kwa sasa serikali imepanga kufufua usafiri huo kuwa kama wa barabara.

Alisema wako kwenye mpango wa kuandika waraka ambao wataufikisha kwenye baraza la mawaziri na kisha bungeni ili kuruhusu wafanyabiashara kununua mabehewa ya treni kwa ajili ya kusafirishia mizigo yao.

"Wafanyabiashara watakuwa wananunua behewa kwa ajili ya mizigo yao, halafu sisi tutakuwa tunawachaji gharama ya kutumia reli yetu, lengo ni kutaka sekta hii ifike mbali na itumike kwa kiwango kikubwa kuongeza uchumi wa nchi," alisema.



Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri la Tanzania, Anna Makinda, akimkabidhi kadi ya Bima ya Afya mmoja wa wakazi wa Dodoma, kwenye uzinduzi wa kampeni za uhamasishaji kwa wananchi kujiunga na vifurushi vya bima ya afya uliofanyika leo (jana) mkoani Dodoma. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Udunga. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Mamilioni wenye vitambulisho Nida hawajasajili laini kwa alama vidole

**Na Mary Geofrey**

ZIKIWA zimebaki siku 17 kabla ya kuzimwa laini zote za simu ambazo hazijasaliwa kwa mfumo wa kieletroniki, Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) imebaini watu milioni tatu wana namba za utambulisho wa uraia, lakini hawajajisajili.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu hali ya usajili na vikwazo vyake. Alisema katika watu hao milioni tatu wenye namba za vitambulisho, wanatarajiwa kusajili laini milioni 5.6 kwa kuwa mtu mmoja anamiliki laini zaidi ya moja. "Laini zilizosajiliwa kwa ujumla ni 47,063,603 hadi kufika Desemba 10, mwaka huu, ambazo zinamilikiwa na watu milioni 21.1.

"Idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole ni 19,681,06 sawa na asilimia 42 ambazo zinamilikiwa na watu milioni 7.6," alisema. Mkurugenzi huyo alisema idadi ya watu wenye namba za usajili, lakini hawajajitokeza kujisajili, inatokana na kukosa uelewa wa kutumia namba ya kujisajili na namna ya kutambua namba za vitambulisho vyao.

Aliwataka Watanzania waliojisajili kwa alama za vidole, lakini hawajapewa vitambulisho, kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda 15096 na kuandika jila kwanza, jina la mwisho, tarehe, mwezi na mwaka wa kuzaliwa, jina la kwanza la mama na jina la mwisho la mama ili kupata namba ya usajili kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida).

Alisema njia ya pili ya kutumia ili kufahamu namba hizo ni kupiga *152*00# kisha kuchagua namba 3 (ajira na utambuzi).

Kilaba alisema njia ya tatu ni kutumia anuani ya https://services.nida.go.tz/nidaportal/get_nin.aspx kupata namba ya usajili kutoka Nida.

"Kila Mtanzania aliyejisajili anapaswa kutumia njia hizi ili kupata namba yake ya usajili na kwenda kusajili laini zake na kama atakutana na matatizo kadhaa, basi anapaswa kufuata maelekezo ikiwamo ya kukumbuka jina la mzazi na namba aliyojisajilia Nida," alisema Kilaba.

Aprili 26, mwaka huu, Rais John Magufuli, akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Mbeya, aliitaka TCRA kuanza usajili kwa mfumo wa kieletroniki ili kuwalinda watumiaji dhidi ya matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano ya simu nchini.

Alisema lengo ni kuwawezesha watumiaji kutambuliwa kama wanatumia huduma za kuongeza thamani kama vile huduma za benki kupitia simu za mkononi, uhamisho wa fedha kwa njia ya simu za mkononi, malipo ya kitamtandao kwa huduma kama za umeme, maji na ada za shule.

Dhumuni lingine ni kuimarisha usalama wa watumiaji na kuwezesha waendeshaji wa mtandao kuwahudumia wateja wao kwa usalama.

Mei Mosi, mwaka huu, TCRA walianza rasmi kazi ya usajili kwa alama za vidole kwa kushirikiana na kampuni za simu za mikononi na kazi hiyo itafungwa rasmi Desemba 31, mwaka huu saa 6:00 usiku na mtumiaji wa simu ambaye hatajisajili laini yake, itakuwa imefungwa rasmi.

# DC aagiza kila mtu alime ekari mbili

**Na Tiganya Vicent,** KALIUA

KILA mkazi wa Wilaya ya Kaliua mwenye uwezo wa kufanya kazi, ametakiwa kuhakikisha analima ekari moja ya zao la chakula na nyingine ya zao la biashara msimu huu ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kutokomeza umaskini.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, katika ziara ya kuhimiza wananchi kushiriki katika kilimo cha mazao ya chakula na biashara katika vijiji mbalimbali wilayani humo.

Alisema mpango wa wilaya ni kuhakikisha wanahimiza kila mwanakaya mwenye uwezo wa kufanya kazi, anakuwa na shamba lisilopungua ekari mbili ikiwa na zao la chakula na biashara ili uzalishaji wa mazao hayo uongezeke na kuiwezesha halmashauri kupata mapato yanayotokana na mauzo ya mazao ya biashara.

"Tunataka mwaka huu kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, alime ekari moja ya zao lolote la chakula na ekari nyingine alime zao lolote la biashara, ikiwa pamba sawa, ikiwa korosho sawa, na ikiwa tumbaku sawa," aliagiza.

Aliwataka wakulima kuhakikisha wanalima kilimo kinachozingatia kanuni za kilimo bora ikiwamo kufanya palizi mapema na kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu.

Pia, aliwataka wakulima kutumia fursa iliyotolewa na serikali ya mkulima kutowekewa vikwazo katika uuzaji wa mazao yake.

Vilevile, kiongozi huyo wa wilaya, alitoa wito kwa wakazi wa eneo hilo kuhakikisha wanasomesha watoto wao ili siku za baadaye watoe msaada kwao ikiwa ni pamoja na kuelimisha juu ya kilimo bora.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA PLC** Tutauza kwa **MNADA WA HADHARA** dhamana ya mikopo ya mdaiwa wa Benki ambayo ni **NYUMBA KWA AJILI YA MAKAZI/BIASHARA**. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | ADWEST COMMUNICATION (T)LTD/ PROJEST KATABAZI SHUMBUSHO | KIWANJA NA, 2043/11, HATI NA 108510, KITALU "L" ENEO LA MBEZI BEACH MANISPAA YA KINONDONI | 28/12/2019 |

**Masharti ya Mnada:**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**

Mkurugenzi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/766-309913

AU

Mkurugenzi Mtendaji
BANK OF AFRICA PLC
NDC Development
Ohio Street/Kivukoni Front
P.O.BOX 3054
DAR ES SALAAM
TE: +255 2110104/2111290



MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | HAWA LEONARD MLUNYA (TAWI LA AGGREY) | HAWA LEONARD MLUNYA | KIWANJA KILICHOENDELEZWA KILICHOKO MTAA WA MAKABE – WILAYA YA UBUNGO | 30/12/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | SALMA HASSAN RAJAB (TAWI LA TEMEKE) | SELEMANI KAFOKOMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO MBEZI MSAKUZI – WILAYA YA UBUNGO | 30/12/2019 SAA 12:00 MCHANA |
| 003 | MWAJUMA SHAIBU SELEMANI (TAWI LA KARIAKOO) | MWAJUMA SHAIBU SELEMANI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MBEZI MSAKUZI - WILAYA YA UBUNGO | 30/12/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 004 | EVA JOHN MIHAYO (TAWI LA AGGREY) | DIDAS DONATUS NYAKIMWE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA CHANIKA – WILAYA YA ILALA | 03/01/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 005 | ESTHER JAMES TENGA(TAWI LA TANDALE) | ESTHER JAMES TENGA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KIBAHA MAILIMOJA– WILAYA YA KIBAHA | 07/01/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 006 | BETHUEL NAFTALI KIWOLI(TAWI LA MAKAO MAKUU) | BETHUELI NAFTALI KIWOLI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA – WILAYA YA UBUNGO | 07/01/2020 SAA 08:00 MCHANA |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 669,
DAR ES SALAAM
Tel+255 02221183403

AU

Maseto Auctioneer,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU
+255 762 260 787

115555902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kili Stars, Zanzibar Heroes msituangushe Cecafa leo

**MICHUANO** ya Kombe la Chalenji kwa upande wa Kundi B, inatarajiwa kuendela leo kwa kuchezwa mechi mbili za kuhitimisha hatua hiyo ya makundi ambazo zitatoa timu moja itakayoungana na Kenya kutinga nusu fainali.

Katika michuano hiyo ambayo washindi wawili kutoka katika kila kundi watatinga nusu fainali, Kundi A linaundwa na wenyeji Uganda, Burundi, Eritrea, Somalia na Djibouti wakati Kundi B mbali ya Kilimanjaro Stars na Zanzibar Heroes, pia zimo Kenya na Sudan.

Kwa upande wa Kundi A, tayari wenyeji Uganda wameshafuzu na watajua timu itakayoungana nayo kwenda hatua ya nusu fainali baada ya mechi zao za kesho, Jumapili.

Mechi za leo zinatarajiwa kuikutanisha Kilimanjaro Stars yenye alama tatu dhidi ya Sudan ambayo ina pointi moja sawa na Zanzibar Heroes itakayovaana na Kenya yenye pointi sita kileleni mwa Kundi hilo la A.

Hivyo, timu zote tatu, Kilimanjaro Stars, Zanzibar Heroes na Sudan, zina nafasi ya kufuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Hesabu zinaonyesha endapo Kilimanjaro Stars itaibuka na ushindi dhidi ya Sudan itafikisha alama sita ambazo haziwezi kufikiwa na Zanzibar Heroes hata kama itashinda dhidi ya Kenya leo.

Lakini pia, endapo Kilimanjaro Stars itapoteza na wakati huo huo Kenya ikashinda ama kutoka sare dhidi ya Zanzibar Heroes, moja kwa moja Sudan itafuzu kutokana na kufikisha alama nne hivyo kuipiku miamba hiyo miwili ya Tanzania.

Kwa Zanzibar Heroes nafasi yao ya kufuzu nusu fainali inategemea endapo tu itashinda dhidi ya Kenya kwa idadi kubwa ya mabao huku ikiombea Kilimanjaro Stars itopoteze kwa mabao machache dhidi ya Sudan, hivyo kulingana pointi na Wasudan hao ili linapokuja suala la tofauti nzuri ya mabao, Zanzibar iweze kunufaika.

Ilivyo ni kwamba, endapo Sudan itashinda na wakati huo huo Zanzibar Heroes ikaichapa Kenya, zote zitafikisha alama nne, hivyo timu yenye tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa itafuzu kutokana na miamba hiyo ilipokutana ilitoka sare ya bao 1-1.

Hali hiyo ndiyo inayofanya mechi hizo kuonekana kama fainali, kwani Kenya tu ndiyo itakuwa haina cha kupoteza kutokana na kutaka kulinda heshima leo kwa kushinda mechi zote za hatua ya makundi, wakati zingine zikiwania ushindi ili kuweza kuungana nayo kutinga nusu fainali.

Aidha, kutokana na Kenya kutokuwa na chakupoteza leo kwa kuwa imeshatinga nusu fainali, inaweza kuutumia mchezo huo kwa kutoa nafasi kwa wachezaji wake ambao walikuwa hawakupata nafasi ya kucheza kwenye mechi zilizopita, hivyo kuwa rahisi kwa Zanzibar Heroes kushinda.


Kwa mantiki hiyo, presha kubwa itakuwa kwa Kilimanjaro Stars ambayo inahitaji ushindi wakati huo huo mpinzani wake, Sudan naye akihitaji kushinda ili kutinga nusu fainali.

Hivyo, si mechi rahisi kwa pande zote, lakini Nipashe hatuna shaka yoyote kuelekea mchezo huo kwa kuwa tunaamini kama ambavyo kocha wa Kilimanjaro Stars, Juma Mgunda, alivyoeleza jana kuwa amezifanyia kazi kasoro zilizojitokeza kwenye mechi zilizopita, wachezaji watatekeleza kile walichoelekezwa wakiwa dimbani leo.

Lakini pia, tunazidi kuamini kwamba Mgunda ameisoma vema Sudan baada ya kuishuhudia wakati ikitoka sare dhidi ya Zanzibar Heroes katika mechi yao ya awali, ingawa hilo haliwezi kutufanya kujiaminisha sana kwani hata wapinzani wao watakuwa waliisoma vema ikicheza na ndugu zao wa Zanzibar.

Jukumu letu kama Watanzania ni kuendelea kuelekeza dua zetu kwa Kilimanjaro Stars, lakini pia kwa Zanzibar Heroes ili timu mojawapo iweze kurejea na ubingwa huo nchini, tunaamini wachezaji wataitendea haki dhamana ya kuivaa jezi ya taifa kwa kushinda katika mechi hizo za leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Matumizi ya klabu yakaguliwe

Na Barnabas Maro

**'KLABU'** ni kundi la watu walioungana hasa kwa ajili ya michezo; jengo au mahali wanapokuta wanachama wa michezo. Makao ya wanachama wa jumuiya ya michezo. 'Ungana' ni kushirikiana na watu wengine ili kufanya kwa pamoja shughuli, kama vile siasa, biashara, michezo n.k.

'Fadhila' ni jambo jema ambalo mtu humfanyia mwingine; hisani, ukarimu, wema. 'Fadhili' ni fanya hisani, saidia mtu; -pa mtu asiye na uwezo fedha za kutatua shida.

Mwaka 1935 Yanga na Simba zilikuwa moja, lakini zilitengana na kuundwa timu iliyoitwa Sunderland ambayo sasa ndio Simba. Klabu hizi kongwe (-enye kuzeeka sana, -a zamani) vimeshindwa kabisa kujitegemea tangu vilipoundwa.

Kwa kiasi kikubwa, tangu Yanga ilipoundwa mwaka 1935 imekuwa tegemezi (-enye kutumainia kiumbe kingine kwa mahitaji yake) mno kwa Wahindi.

Kadhalika, Simba iliyoundwa mwaka 1936 baada ya kutengana na Yanga, kwanza iliwategemea Waarabu kisha Wahindi.

Katika wote hao anayeelekea kuinufaisha Simba zaidi ni bilionea kijana aitwaye MO Dewji. Huyu ameijengea uwanja wa kisasa wa mpira na kuifanya Simba kuwa na uongozi wa ngazi zote muhimu kama zilivyo timu za Ulaya.

Kwa Yanga, Mhindi wa mwisho kuifadhili alikuwa Yusuf Manji. Huyu alikuwa kila kitu kwa Yanga na alipojiuzulu, umuhimu wake ukaonekana wazi kuwa ndiye aliyekuwa uhai wa Yanga.

Kwanza alitaka kuifanya Yanga iwe kama klabu za Ulaya, kwa kutangaza biashara zake kupitia klabu hiyo kama zifanyavyo kampuni za Ulaya kwa klabu za huko.

Hata hivyo, baadhi ya viongozi waliokuwa chini yake walitumia nafasi hiyo kujinufaisha (wenyewe husema 'kupiga hela'). Huo ukawa mwanzo wa Yanga kuporomoka. Wajanja wakajinufaisha kwa fedha za Manji na klabu.

Sasa Yanga imedhoofika (kitendo cha jambo au hali kupungua nguvu au uwezo wake). Imekuwa hohehahe, yaani maskini sana. Yashindwa kulipa mishahara ya wachezaji na hiyo imesababisha baadhi ya wachezaji kuvunja mikataba yao na kuondoka!

Ingawa wameondoka, isidhaniwe kuwa wamesamehe mishahara na fedha zao za usajili, hasha! Wataendelea kudai kwa kupeleka malalamiko yao TFF na ikibidi hata Fifa kama Yanga ikishindwa kuwalipa. Fedheha iliyoje!

Kitendo cha wachezaji kuishitaki Yanga kwa kutolipwa haki zao kinawakatisha tamaa wachezaji waliopo na kuifanya klabu kuwa na hali ngumu ya kupata wachezaji wengine muhimu.

Wachezaji wanne muhimu kutoka nje ya nchi waliokuwa wasajiliwe na Yanga, walitwaliwa dakika za mwisho na Simba. Sasa ndiwo vinara wa timu hiyo kwa uchezaji na ufungaji. Wakati Yanga wakitaka kusajili kwa maneno, Simba huenda na fedha taslimu mkononi. Nani atakataa?

"Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Yanga wanapaswa kukubaliana na methali hii kwani wakati walipowasajili wachezaji wa ndani na nje Kwa gaharama kubwa, kufanya mazoezi yao ughaibuni na kutokuwa na ukata (umasikini uliopindukia mpaka; ufukara) waliwacheka sana watani zao (Simba).

Niwakumbushe Yanga methali inayotahadharisha na kuonya kuwa "Fedheha za mwenzio, usizifurahie." Maana yake si tabia njema kufurahia aibu au fedheha zilizomfika mwenzako.

Twahimizwa umuhimu wa kutowacheka wengine wanapopatwa na matatizo kwa kuwa nasi tunaweza kupatwa na matatizo hayo hayo. Leo ni kwao, kesho ni kwetu.

Yanga twakumbuke walivyowacheka Simba wakati walipokuwa kwenye ukata! Vijana wa mjini husema "Kutesa kwa zamu." Ilivyo sasa ni zamu ya Simba kuicheka Yanga. Waingereza husema 'tit for tat' yaani 'nipe nikupe; jicho kwa jicho.'

Kuna kila dalili kuwa ukata wa klabu husababishwa na baadhi ya wanachama wanaogombea uongozi si kwa lengo la kuongoza bali 'kujiongeza.' Wenyewe wana usemi wao kuwa kula hela za klabu ni 'kupiga hela!' Wanajua namna hela 'zinavyopigwa.' Kwa nini wasiseme wazi kuwa ni jinsi hela zinavyoibwa/ibiwa?

Badala ya kwenda na mawazo ya jinsi ya kukuza mapato ya klabu, wao hugombea nafasi za uongozi kwa lengo la kuiba fedha chache za wanachama. Badala ya kuwa na mikakati ya kusajili wanachama, wao hufikiria namna ya kujinufaisha!

Tena hufanya kwa bidii sana ili wakikosa kuchaguliwa uchaguzi ujao wawe na ukumbusho wa mambo waliyochuma walipokuwa viongozi.

Kwa ujinga na tamaa za kutaka kujinufaisha, wezi hao wasiokuwa na haya husema: "Kufa kwa wengi arusi." Kwamba kufa kwa watu wengi hakusikitishi sana kwani ni kama arusi.

Methali hii huweza kutumiwa kushauri kwamba jambo baya litokeapo kwa watu wengi ni afadhali kuliko kwa mtu mmoja. Kwa tafsiri yao, ni bora wanachama wa Yanga wadhurike kuliko adhurike kiongozi mmoja anayetafuta ulaji kama wasemavyo wenyewe, 'kupiga hela.'

HABARI KITAIFA

# Wataka adhabu ya viboko ifutwe

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa shule mbalimbali za sekondari nchini, wameishauri serikali kufuta adhabu ya viboko na adhabu zingine katili kwa wanafunzi kwani zinawasababishia madhara makubwa.

Walitoa maoni hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mjadala wa kuhamasisha usalama shuleni ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizofikia tamati hivi karibuni.

Mjadala huo uliandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika, (WilDAF) kwa kushirikiana na Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (Vipamaru).

Lengo la mjadala huo, kwa mujibu wa Menaja Ushawishi na Utetezi wa WiLDAF, Neema Meremo, ulilenga akutafuta namna ya kuweka mazingira salama na rafiki katika shule mbalimbali nchini.

Mwanafunzi Maliki Abdurahman wa Shule ya Sekondari Tandika, alisema baadhi ya walimu wamekuwa wakitoa adhabu zinazodhalilisha na kuumiza wanafunzi.

Alishauri mwanafunzi anapokosa walimu wakae naye kuzungumza namna ya kurekebisha tabia yake badala ya kutumia viboko kama njia pekee ya kumrekebisha.

Mwanaidi Fais wa sekondari ya Makumbusho alisema viboko shuleni si suluhisho la kurekebisha tabia za wanafunzi kwani baadhi wamekuwa sugu kutokana na mazoea ya kupigwa kila wakati.

"Ni kweli kuna wanafunzi wakorofi lakini kuna mwalimu akimpiga mwanafunzi unaweza kudhani anapiga mwizi sasa sisi hatuoni kama ni sawa. Kuna adhabu mbadala za kumjenga mwanafunzi kitaaluma zinaweza kutumika na mambo yakaenda vizuri tu," alisema. Miriam Katara wa sekondari Mzimuni alisema mara nyingi adhabu kubwa zinazotolewa na walimu wala hazilingani na makosa yaliyofanywa na wanafunzi.

"Unakuta mwanafunzi ameongea darasani sasa adhabu anayopewa unaweza kudhani amefanya jambo kubwa sana kwanini wasitafute adhabu mbadala na kuna nchi ambazo hakuna viboko na wamefaniiwa kurekebisha tabia za wanafunzi twene tujifunze wamefanikiwaje," alisema

Noela Elias wa Turiani, alisema kwenye shule yao walimu wamekuwa wakitoa adhabu kali kiasi kwamba mwanafunzi anaweza kushindwa kuja shule siku inayofuata kutokana na maumivu.

"Mwalimu mwingine anawaweka juani kwa muda mrefu na kuwarusha kichura chura mwingine anaweza kuwalaa juani kifudi fupi sasa inaumiza sana watafute adhabu mbadala za kujenga badala ya hizi za sasa," alisema

# Wagonjwa 200 wafikishwa hospitali Mirembe kila siku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Hospitali ya Mirembe, Dk. Erasmus Mndeme, amesema asilimia 75 ya wagonjwa wa akili wanaohudumiwa katika hospitali hiyo ni wanaume.

Dk. Mndeme aliyasema hayo jana alipozungumza na timu ya maofisa habari wa wizara na taasisi zake mkoani Dodoma iliyotembelea hospitali hiyo kwa lengo la kuangalia mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Alisema asilimia 99 ya wagonjwa wa akili (450) wamelazwa huku Taasisi ya Itega ikihudumia wagonjwa wa dawa za kulevya 310 ambao wanafika kila siku kupata dawa.

"Wagonjwa 200 hadi 300 kwa siku wanahudumiwa kwenye Hospitali ya Mirembe ikiwamo wagonjwa wa akili na wagonjwa wa kawaida ni kidogo. Kwa mwaka mzima, tunafikia wagonjwa 230,000," alisema.

Akizungumzia miaka minne ya Rais Magufuli, Mkurugenzi huyo alisema hospitali hiyo na Taasisi ya Isanga imefanikiwa kufanya mambo makubwa 11 ikiwa ni pamoja na ukarabati uliogharimu Sh. milioni 980 kwa kukarabati wodi 10.

"Pia tulikarabati jengo letu la nje linalohudumia wagonjwa wa akili, na pia mashine ya X-ray, tumekarabati chumba cha upasuaji, dawa na ukarabati mwingine mdogo," alisema.

Alisema kwa kipindi hicho, hospitali imenunua mashine mbili za kupima mkojo ambazo zimegharimu Sh. milioni 44.

"Pia, kipindi hiki hospitali imefunga mfumo mkubwa wa kielektroniki wa kuboresha makusanyo ya hospitali, na umefungwa pia Kituo cha Itega na Taasisi ya Isanga inayohudumia wagonjwa wa akili wafungwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi hicho, kimefunguliwa kitengo cha kisasa cha kitaaluma cha kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya ambacho kwa sasa, wagonjwa 320 wameandikishwa na wanatumia dawa ya methadone.

"Mafunzo ya kuhudumia wagonjwa wa akili wakorofi yametolewa kwa watumishi 170, lakini kwa awamu hii tumefundisha watumishi 36, haya ni mafunzo maalum tumeyatoa Uingereza ili kukabiliana na wagonjwa wa aina hii," alisema.

Aliongeza kuwa wamefungua kliniki tatu za kibingwa ambazo ni wazee, watoto na watu wenye msongo mkubwa wa mawazo.

"Hospitali imeongeza makusanyo katika kipindi hiki kutoka Sh. milioni 350 hadi 680, ni mara mbili zaidi na hii imetokana na kufungwa na kutumia mfumo huu," alisema.

Kuhusu dawa, alisema serikali imetoa mgawo wa dawa wa Sh. bilioni 2.3 na kufanikisha upatikanaji wa dawa kwa asilimia 95 hadi 98 kwa dawa za magonjwa ya akili ambazo zipo za aina saba.

Maofisa hao pia walitembelea Chuo cha Uuguzi Mirembe ambacho kwa sasa kina wanafunzi 400.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola (kushoto), akisalimiana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba John Kabudi, Uwanja wa Ndege wa Mwanza jana. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Suza yatinga shindano mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHUO Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA), kimebahatika kuingia kwenye shindano la 'Mabadiliko ya Tabianchi' lililoandaliwa na Umoja wa Mataifa likiwa na lengo la kuleta mabadiliko katika jamii.

Shindano hilo linatarajiwa kufanyika kwa awamu ya kwanza leo (Disemba 14) katika ukumbi wa chuo za SUZA Vuga mjini Unguja.

Akizunguza na waandishi wa habari hizi, Kiongozi wa Serikali ya wanafunzi kutoka Chuo hicho kwa upande wa Pemba, Mohamed Ali Abdi, alisema shindano hilo ni fursa kwao na jamii kwa ujumla.

Alieleza lengo ni kuleta mabadiliko katika jamii ambapo wanafunzi hupewa nafasi ya kutambulisha mawazo yao juu ya jambo fulani ambalo hutangazwa kila mwaka na Umoja wa Mataifa.

"Jambo hilo litasaidia kutoa msaada katika Dunia tutakayoijenga katika miaka ya mbele, shindano hilo linalenga mabadiliko ya tabianchi ambayo ni moja katika ya malengo endelevu ya Umoja wa Mataifa," alisema Mohamed.

Alisemaa anaamini shindano hilo litaleta mabadiliko chanya, kwani wataweza kufikisha maoni yao katika Baraza la Umoja wa Mataifa, jambo ambalo ni kuitangaza Zanzibar na kuiletea maendeleo.

"Tunataka tukabiliane na mabadiliko ya tabianchi, kwani imekuwa mbaya sasa, maeneo mengi yameshakumbwa na hali hiyo, hivyo tunaamini kuwa shindano hili litaleta tija kwa jamii yote nzima," alisema.

Naibu waziri wa Elimu wa Serikali ya wanafuzi wa chuo hicho, Pemba, Mohammed Ali Mohammed, alieleza kuwa shindano hilo litawanufaisha sana kwani watapata uzoefu, kujitolea, kujiamini na kuelewa kwa upana kuhusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana nayo.

"Tunaomba wananchi washiriki katika shindano hilo na watoe mawazo yao, yatakayowajengea uwezo zaidi kwa kile watakachokwenda kukieleza nje ya nchi, kwani mabadiliko ya tabianchi yanaathiri siku hadi siku duniani kote," alieleza.

Nae, Naibu Katibu wa Umoja wa Vijana wa Mataifa kupitia SUZA Pemba, Abdul-latif Soud Mussa, alisema ipo haja kwa vijana kushiriki katika shindano hilo la ili kuleta mabadiliko chanya kwa jamii.

# Wanaswa kwa tuhuma ukeketaji wasichana

**Na Rose Jacob,** TARIME

WATU 53 wilayani Tarime, mkoani Mara, wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuwakeketa wasichana na kuwatahiri watoto 200 na kuongeza uwezekano wa kuambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU). Watuhumiwa hao walikeketa mabinti 15 na wengine kuwafanyia tohara kwa watoto wa kiume 200 kwa kutumia visu nane.

Akizungumza na wanahabari, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri alisema tohara hizo za mwaka 2019 zimeambatana na mauaji ya Mwalimu wa Sekondari ya Itile wakati mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule hiyo amekatwa mkono.

"Vitendo hivi vya kikatili vimekuwa vikifanywa na vijana ambao wanajiandaa kufanya tohara, kabla ya shule kufungwa. Inadaiwa waliingia katika shule mbili na kulazimisha watu wawapate fedha. Aidha , Novemba 14 mwaka huu vijana hao walimuua mwalimu huyo kwa kumchoma na mkuki shingoni.

"Watuhumiwa hao watano waliofanya unyama huo wameshakamata, wengine watatu wametorokea nchini Kenya na sisi tumefanya mawasiliano na wenzetu wa Kenya tutawakamata tu,"alisema Msafiri.


Alieeleza kuwa watu 29 wamefikishwa na waliobaki watafikishwa mahakamani upelelezi ukikamilika na kwamba kati yao 27 ni wanawake na 26 ni wanaume, wakiwamo wawili mmoja aliyetumia visu nane kutahiri watoto 200.

"Ukeketaji huu ni mkubwa sana na unasaidiwa na wazee wa kimila ingawa wengi wamepewa maelekezo na semina nyingi kuhusu kuacha ukeketaji na tohara zisizo salama, lakini bado hawataki kubadilika, kama mtu hataki kujierekebisha tutamkamata na kufikisha katika vyombo vya sheria na tutahakikisha adhabu kali inatolewa kwa mujibu wa taratibu na sheria,"alionya Msafiri. Alisema watoto 15 waliokeketwa wengi wao hali zao zilikuwa mbaya na ili lazimika kuwapeleka hospitali kwa ajili ya matibabu maana damu nyingi zilikuwa zikiwatoka.

Alisema baada ya huduma hali zao ziko vizuri na tayari wako katika kituo cha Association For Termination of Female Genital Mutilation (ATFGM) kilichoko wilayani humo.

Aidha, alionya kuwa serikali haitakubaliana na vikundi vya watu wachache wanaotaka kuleta madhara ndani ya jamii na kuahidi kuwa watawashughulikia na wanaojihusisha na tohara zisizo salama waache mara moja kwani wananchi wanahitaji Tanzania iliyo na raia wenye afya njema.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo cha kuwalelea watoto ambao wamekimbia ukeketaji cha ATFGM cha Masanga, Sisita Stella Mgaya, alisema wamekuwa wakikutana na ukinzani mkubwa kutoka kwa wazee wa mila, ambao wanaona asasi hiyo inakwenda kinyume na mila na desturi zao hasa kwenye suala la ukeketaji.




Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Temeke Dar es Salaam, Dk.Serafini Patrice (kushoto), akipokea moja ya mashine zenye thamani ya Sh. milioni 12.6 ijulikanayo kwa jina la Patient Monitor, inayofuatilia mwenendo wa afya ya mgonjwa kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Swissport International, Yassin Mrisho, juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Familia maskini zapewa funzo kuondoa ufukara

**Na Mwandishi Wetu, NZEGA**

MKUU wa Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, Godfrey Ngupula, amewataka wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wilayani humo kutumia ruzuku kujiondolea umaskini.

Aidha, amewataka kuzitumia ruzuku wapewazo kikamilifu ikiwamo kujishugulisha na kilimo hasa katika kipindi hiki cha masika ili kujikwamua na umaskini.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa nasaha kwa wanufaika wa mpango huo wa Tasaf wa Kijiji cha Nzogolo, waliokuwa wakipatiwa fedha za kunusu kaya maskini.

Aliwataka kuzitumia fedha za mpango huo walizozipata kwa shughuli za kilimo kwa kulima mazao mbalimbali hasa pamba na mpunga kwani yanastawi zaidi katika maeneo yao na kuongeza kuwa kilimo ndicho kitakachowasaidia kupata mazao mengi na ya chakula na biashara.

Mkuu wa wilaya aliwapongeza wale wote wanaozitumia fedha hizo vizuri kwa kulima, kusomesha watoto, kujenga nyumba bora na kufuga na kwamba wanapofanya hivyo ni akiba yao ya baadaye ya kuendelea kujiondoa katika umaskini.

Kadhalika aliwakemea ambao bado wana matumizi mabaya ya ruzuku za mpango huo ikiwamo wanaume ambao huzilewea.

Wanufaika wa mpango huo wa Tasaf wa kijiji hicho cha Zogolo, Peter Masanja na Amina Abbas waliishukuru serikali ya wamu ya tano kwa kuendeleza mpango huo tangu ulivyoanza mwaka 2015 wa kuhawilisha fedha katika kaya maskini na kuongeza kuwa wamewezeshwa kununua mifugo, kusomesha watoto na kwa sasa wanajikita katika kilimo ili waendelee kuinuka kiuchumi.

Ofisa ufatiliaji wa mpango huo katika wilaya ya Nzegam, Zahara Mbailwa, alisema katika wilaya hiyo kuna kaya 700 zinazonufaika na mpango huo wa awamu ya tatu na kuongeza kuwa mpango huo ulisimama kuanzia Machi mwaka huu kutokana na kuhama awamu ya kuingia ya pili.

Alitoa wito kwa wanufaika wote wilayani Nzega kuendelea kuutumia vizuri ikiwamo kilimo hasa katika kipindi hiki cha masika.

## Balozi ataja mbinu kufanikiwa kimaisha

**Na Juster Prudence**

WASICHANA wameshauriwa kuwa na uthubutu jambo litakalowasaidia kupigana na umaskini na malezi hafifu kutoka katika familia zao na baadaye kufikia malengo yao.

Akizungumza katika mkutano wa mpito wa wasichana wajasiriamali jana jijini Dar es salaam, Kaimu Balozi wa Marekani, Dk. Inmi Patterson, alisema uthubutu ndiyo njia pekee inayoweza kumsaidia msichana kutimiza au kufikia malengo yake na kuepukana na umaskini.

Kwa mujibu wa Inmi, kila msichana ana ndoto ya kuwa na maisha huru ya kujitegemea ambayo yatamsaidia kukidhi mahitaji yake na maisha hayo yatawezekana kama wasichana watapata elimu, ujuzi pamoja na uthubutu utakaosaidia kuboresha mawazo yao.

Alisema wasichana wana haki sawa kama watu wengine ili wapate nguvu ya kujituma zaidi katika kuwa wajasiriamali na kuongeza kuwa wanatakiwa kuwa na mawazo chanya ya kibiashara pamoja na mawazo ya kusaidia jamii yatakayoweza kuleta usawa na kutokomeza umaskini.

Kaimu Balozi alisema kuwa Marekani iko tayari kuwawezesha wasichana wa Tanzania watakaokuwa na mawazo mazuri ya kibiashara au hata ya kijamii ambapo kwa mwaka huu wa 2019 wametoa msaada wa Dola 10,000 kwa Zahara Mohamed ambaye ni mhitimu wa kidato cha nne anayejihusisha na kupinga unyanyasaji kwa watoto wa kike.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kutetea Haki za Wasichana(msichana initiative), Rebecca Gyumi, aliwataka wazazi kuacha matabaka katika malezi wanayotoa kwa watoto wa kike badala yake wawape malezi sawa na watoto wengine ili kuwaongezea uwezo wa kujiamini kukuza mawazo yao na kufikia ndoto zao.

Aidha, aliwataka wasichana kuwa na umoja, kusaidiana na kupendana ili waweze kufikia ndoto zao na malengo ya taifa badala ya kujenga chuki za wao kwa wao.



Mkazi wa Kijiji cha Lengast, Kata ya Naisinyai, mkoani Manyara, Roza Lembris, akielezea changamoto ya miundombinu ya barabara na mawasiliano kwenye mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, kwa mhandisi Zephania Chaula juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mvua yakata mawasiliano vijiji vinne

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MVUA zinazoendelea kunyesha mkoani Arusha zimesababisha kukatika kwa mawasiliano katika vijiji vinne vilivyoko kata ya Engaruka wilayani Monduli, hatua ambayo imewafanya baadhi ya wasafiri kulala njiani kwa siku kadhaa.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddi Kimanta, alisema hayo juzi baada ya kutembelea baadhi ya maeneo yalioathirika na mvua katika kata hiyo.

Alisema kutokana na tatizo hilo, wanaendelea na jitihada za kuweka vifusi kwenye baadhi ya maeneo ili kuunganisha mawasiliano wakati jitihada zingine zikifanyika. Kimanta alisema mvua zinazoendelea kunyesha mkoani hapa, zimesababisha uharibifu mkubwa ikiwamo miundombinu ya barabara ambayo ndio kiungo kikuu cha mawasiliano Kutoka Loliondo kwenda jijini Arusha.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Wilayani Monduli, Mhandisi Janeth Mhokera, alisema mvua hizo zimesababisha uharibifu mkubwa kwa kukata mawasiliano kwenye vijiji hivyo. Alisema jitihada zinazoendelea kwa sasa ni kuboresha miundombinu iliyoharibika.

"Ili kurejesha mawasiliano ya vijiji hivi, wahandisi wako maeneo yaliyokumbwa na tatizo hilo kwa ajili ya kumarisha barabara zote katika wilaya hii," alisema Janeth.

Naye Mtendaji wa Kijiji cha Eleendeli, Feli Mkwabi, alisema kwa sasa hali ni mbaya kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani hapa hasa katika kata hiyo.

Alitaja vijiji vilivyoathirika kuwa ni Engaruka Juu, Engaruka Chini, Irendeni na Oldonyo na kuongeza kuwa mbali na mvua hizo kuharibu mazao na barabara, zimesababisha baadhi ya mifugo kufa kutokana na kusombwa na mafuriko.

Wakizungumza kwa niaba ya wananchi wengine, Elia Laizer na Neseri Lazaro walisema mbali na miundombinu ya barabara kuharibika na mvua pia imeharibu ekari za mazao yao shambani.

"Kuharibika kwa mazao haya na kusombwa kwa mifugo yetu kumesababisha vifo vya mifugo yetu, hali iliyoturudisha nyuma jitihada za kujikwamua na umaskini,"alisema.

Wameiomba serikali kuwapelekea mbegu ili warudie kupanda katika mashamba yao baada ya kusaidiwa kutoa maji yaliozingira mashamba yao.

# Wanafunzi sekondari, vyuo wapewa elimu uhifadhi

**Na Daniel Sabuni,** ARUMERU

WALIMU wa Shule za sekondari na vyuo kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, wamepewa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na utunzaji wa mazingira.

Akizungumza jana katika mafunzo hayo yanayofanyika jijini hapa, Mratibu Mkuu wa Malihai kutoka Mamlaka Udhibiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), Benjamin Kijika, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo kuhusiana na mali hai zilizopo nchini na kuwahamasisha wanafunzi kutambua umuhimu wake. "Ukimwelimisha mwalimu umeelimisha taifa zima. Hawa wakishafundisha jambo kwa wanafunzi, ujue taifa zima limeelimika. Lazima tuwe makini na maliasili zetu. Tufahamu kuwa zinatuletea fedha za kigeni kutokana na kuwa kivutio kwa watalii," alisema.

Alisema ongezeko la klabu za malihai katika shule na vyuo nchini limeleta matokeo chanya hususani kwa baadhi ya wanyama ambao waliaanza kutoweka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujangili, lakini sasa elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi na wananchi imesaidia kupunguza ujangili na wanyama hao wameanza kuongezeka.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya, Anaclet Mshashu, alisema walimu wana nafasi kubwa ya kuwajengea uwezo vijana kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema mabadiliko tabia nchi yanatokana na kushindwa kutunzamazingira ambayo huathiri majira na kusababisha kukosekana mvua kwa wakati.

Mshashu alisema mabadiliko ya tabianchi husababisha athari ya majanga ya njaa, vimbunga na kubadili mfumo wa hali ya hewa.

Mmoja wa watumishi wa malihai, Steven Nnko, alisema vijana wakiandaliwa vyema katika uhifadhi wa wanyamapori watakuwa mabalozi wazuri wa kukuza utalii hasa kwa wale wanaopata nafasi za kwenda nje ya nchi kusoma.

Alisema vijana wakifunzwa uhifadhi, wa kulinda wanyamapori na wakiwa wadogo mara wakifika umri wa utu uzima watakuwa mabalozi wazuri wa kuutangaza utalii na vivutio vilivyopo nchini

Baadhi ya waalimu walioshiriki katika mafunzo hayo, akiwemo Beatrice Kitoi na Geofrey Mwakasika, walisema mafunzo hayo yatawaongezea mbinu ya kuwaandaa vijana katika kulinda na kuhifadhi mazingira na viumbe hai.

# Askofu ahimiza Amani na upendo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania(KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Masangwa, amewataka wananchi kuimarisha amani, upendo na mshikamano ili kujenga nchi imara itakayopiga hatua kimaendeleo.

Masangwa aliyasema hayo juzi, wakati akifungua kongamano la kuwanoa zaidi ya wainjilisti 800 na wenza wao lililofanyika jijini hapa.

Alisema ili amani iendelee kuwapo nchini, jamii inapaswa kuimarisha umoja na mshikamano kwa kuwa kutokuwapo kwa vitu hivyo maendeleo hayatakuwapo.

"Watazania wanapaswa kushikamana kuwa wamoja na kumwomba Mungu ili kuwapo amani. Hii amani isipokuwapo hakuna maendeleo yatakayopatikana," alisema Askofu Masangwa.

Askofu aliwataka wainjilisti hao na wenzi wao kufanya kazi ya Mungu kwa bidii na maarifa badala ya kufanya kazi kwa mapenzi na utashi wao ili kujenga taifa ambalo litakuwa na hofu ya Mungu.

"Leo (juzi) tumewakutanisha wainjilisti wote wa dayosisi hii pamoja na wenzi wao lengo likiwa ni kuzungumza nao kuhusu ushirikiano wao wa kikazi na semina hii tumeitoa ili kuwaimarisha wawe wafanisi katika kazi waliyopewa," alisema.

Katibu wa Umoja wa Wainjilisti, Robert Olembaya, alisema wamekusudia kuandaa kongamano hilo ili kujuana na kubadilishana uzoefu wa kikazi, umoja na mshikamano kwa watumishi hao.

Pamoja na kufanya huduma hizo, alisema wamekuwa wakikutana na vikwazo mbalimbali zikiwamo mila na desturi ambazo zimekuwa zikiyumbisha jamii.

# Viwanda misitu vyafundwa ubora

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imeutaka Umoja wa wenye Viwanda vya Mazao ya Misitu Kanda ya Kaskazini (Nofia) kuhakikisha unazingatia ubora wa uchakataji wa mazao hayo ili kushindana katika masoko ya nje.

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa 10 wa wanaviwanda wadogo na wa kati wanaochakata mazao yatokanayo na misitu katika Kanda ya Kaskazini uliofanyika katika ukumbi YMCA mjini hapa.

Prof. Silayo alisema ni vyema wanachama hao wakazalisha kwa ubora ili kupata masoko nje ya nchi na kwamba tayari serikali imeshafanya mawasilianao na Kenya na Zambia ambazo zimekubali kutuma wataalamu kutembelea mashamba hayo kwa lengo la kuingia makubaliano katika uwekezaji na kuweka mkataba ya biashara hiyo.

"Masoko ya mazao ya misitu nje ya nchi yanahitaji bidhaa bora na za hali ya juu. Niwaombe wadau wanaohusika na uchakataji wa mazao haya kuzingatia hilo. Kwa siku za hivi karibuni, tumeshuhudia biashara ya mazao haya nje ya nchi imeshuka kidogo kutokana na kutokukidhi viwango vya ubora," alisema.

Prof. Silayo aliwataka wadau hao kuhakikisha kila mmoja anatoa bidhaa bora zenye ubora huku pia akiwataka wadau hao kuondokana na matumizi ya teknolojia za zamani huku akiwataka kuwekeza kwenye teknolojia mpya zenye kukabiliana na ushindani kwenye soko.

"Tumekuwa na mawasiliano na wenzetu wa Idara ya Misitu ya Zambia ambao wamekubali kutuma wataalamu wao kuja kutembelea mashamba yetu kuona mazao ambayo tunayo na kutaka kukutana na wadau ili kuona namna ambayo wanaweza kuingia makubaliano katika uwekezaji," alisema.

Alisema wafanyabiashara wa mazao ya misitu nchini wamekuwa wakilanguliwa mazao yao na madalali kutoka nchini Kenya kwa kushindwa kuzalisha kwa ubora licha ya kwamba mazao ya nchini yana ubora zaidi na hali ambayo imekuwa ikichangia kushindwa kwenda kuuza mazao hayo nje ya nchi.

"Bidhaa nyingi zinazotoka nje ya nchi ni bora lakini si imara kama zinazozalishwa hapa kwetu. Hii ni kutokana na wawekezaji wa hapa nchini kishindwa kuzalisha kwa ubora kutokana na kukosa mitaji," alisema Prof. Silayo.

Prof. Silayo aliongeza kuwa serikali imeshazungumza na benki ya NMB ili kuangalia kuwakopesha wenye viwanda vya mazao ya misitu ili kununua mitambo ya kisasa ya uchakataji wa mazao hao na hatimaye kuuza nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Nofia, Frank Karonge, alisema wawekezaji wamekuwa wakishindwa kuwekeza kutokana na kupata mikataba ya muda mfupi hali ambayo inachangia kushindwa kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.

Karonge alisema ukosefu wa teknolojia mpya za kisasa imechangia kwa kiasi kikubwa wadau wa mazao ya misitu kuzalisha bidhaa ambazo hazina ubora kutokana na kuendelea kutumia teknolojia za zamani.

# Chuo kikuu chajitosa utetezi wa watoto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHUO Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (Mwecau), kimeanzisha programu mpya ya masomo ya utetezi wa haki za watoto wa vita dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wote wanaojiunga na elimu ya juu.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Philibert Vumilia, alisema jana kuwa kutokana na kuanzishwa kwa program hiyo, hakuna mwanachuo yeyote atakayehitimu elimu ya juu chuoni hapo bila kupitia mafunzo hayo.

Taarifa ya Prof. Vumilia ilithibitishwa jana na Ofisa Uhusiano wa chuo hicho, Athanas Sing'ambi.

"Ni kweli kwamba tumeguswa sana na tatizo la ukatili wa watoto unaoendelea na hasa haki zao kuminywa na mambo yote yanayoendelea kuhusu GBV (ukatili wa kijinsia). Tumesema wafanyakazi na wanafunzi wote hawataruhusiwa kumaliza masoma bila kupitia mafunzo haya ya utetezi wa haki za watoto, " alisema Makamu Mkuu wa chuo hicho.

Alisema kutokana na ongezeko la vitendo vya unyanyasaji kwa watoto katika jamii, Chuo kimeamua kujitosa katika utetezi wa watoto ili kusaidia kupunguza manyanyaso dhidi ya watoto. "Kumekuwa na taarifa mbalimbali zinazoripotiwa katika vyombo vya habari zinazoelezea matukio mbalimbali ya unyanyasaji kwa watoto.

Prof. Vumilia aliongeza kuwa: "Ndiyo maana kabla ya kozi hiyo kuanza, tumeona tuwanoe wahadhiri wote wa chuo kwa siku tatu."

Aidha, Prof. Vumilia alisisitiza mpango huo unalenga kuhakikisha jamii inakuwa salama na kwamba ni lazima ziwapo juhudi za kuwalinda watoto.

"Kwa kuanzia Mwecau tumeamua kuanza kuwaandaa walimu wetu wote kuwa wakufunzi wa masuala ya utetezi wa haki za watoto. Lakini pia wafanyakazi wengine wote na wanafunzi wote hawataruhusiwa kumaliza masoma bila kupitia mafunzo haya ya utetezi wa haki za watoto," alisisitiza.

Alisema baadaye wahitimu hao watapaswa kwenda kuwafundisha jamii katika makundi mbalimbali ili elimu hii isambae maeneo yote yenye viashiria vya unyanyasaji wa watoto.

Msimamizi wa program hiyo, Dk. Peter Siamoo, alisema mafunzo yaliyotolewa yalilenga kuandaa wataalamu wa kufundisha wataalumu wengine (trainer of trainers) watakaofundisha mahali pengine watakapohitajika.

Alikazia kwa kusema mafunzo yameandaliwa kwa lugha zote mbili yaani kingereza na Kiswahili ili kuwafikia watu wengi zaidi katika nchi za Afrika.

Oktoba 23, mwaka huu, serikali ilisema kuna haja ya kufanyika upya tathmini ya kitaifa kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia, baada ya takwimu za utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na serikali ya Tanzania zilizotolewa miaka mitano iliyopita kushindwa kuwa na uhalisia kwa sasa.

Kauli hiyo ilitolewa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii nchini anayefanya kazi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Naftali Ng'ondi.

Ripoti iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wataalam wa Ustawi wa Jamii Tanzania (Taswo), Furaha Dimitrios, inaeleza kuwa hali ni mbaya zaidi katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ambako kati ya Januari na Septemba, mwaka huu, watoto 157 waliripotiwa kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali.

Katika ripoti hiyo, watoto 52 kati ya hao 157 wamefanyiwa ukatili wa kingono ambayo ni sawa na asilimia 33.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara, mhandisi Zephania Chaula (kushoto), akimpongeza meneja wa kampuni ya JB Manga camp, Yohana Manga (kulia), baada ya kampuni hiyo kununua mashine ya kukoboa kwa ajili ya kikundi cha Kiwatemisi cha mji mdogo wa Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Viongozi ushirika kortini tuhuma za wizi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

VIONGOZI wanne wa Chama cha Ushirika wa Mazao (Amcos) cha Manio, wilayani Siha, wamepandishwa kizimbani wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kujipatia Sh. Milioni 60.8 isivyo halali ambazo ni mali ya chama hicho.

Waliofikishwa katika Mahakama ya Wilaya hiyo ni Mwenyekiti wa chama hicho, Remmy Mbando (68), Elisante Kihundwa (55) ambaye ni Katibu, mjumbe Isayi Kileo (70) na wajumbe wa bodi ya chama hicho, Dina Kileo na mmoja ambaye bado hajapatikana.

Mwendesha Mashtaka, Simon Feo, akiwasomea makosa hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Elibahati Petro, alidai washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Januari Mosi, 2017 na Septemba 30, mwaka juu,

Alidai kuwa katika chama hicho, wakiwa watumishi wa chama, washtakiwa isivyo halali na kwa kutumia nafasi zao, waliiba fedha hizo huku wakitambua kufanya hivyo ni kosa.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa washtakiwa wanakabiliwa na makosa hayo mawili ambayo ni kula njama ya wizi kinyume na kifungu cha 384 cha Kanuni ya Adhabu kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Kosa la pili linadaiwa ni wizi wakati wakiwa watumishi kinyume na kifungu 271 cha Kanuni ya Adhabu kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, ikisomwa pamoja na kifungu 126 (1) (h)(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, Namba 1 ya mwaka 2013.

Baada ya maelezo hayo, washitakiwa kwa pamoja walikana mashtaka yanayowakabili.

Muda mfupi baadae, Hakimu Petro alisema dhamani ya washtakiwa iko wazi na kwamba masharti ni kila mmoja kuweka amana ya fedha taslimu Sh. milioni 20.

Hakimu huyo alitaja masharti mengine ni kila mshtakiwa kuwa na hati ya mali isiyohamishika yenye thamani inayozidi fedha zinazodaiwa kuibwa.

Pia kila mshtakiwa alipaswa na mdhamini ambaye ni mtumishi wa serikali mwenye barua kutoka kwa mwajiri wake.

Washtakiwa walishindwa kitimiza vigezo vya masharti ya dhamana na kupelekwa mahabusu. Kesi hiyo imeairishwa hadi Desemba 24, mwaka huu, itakapotajwa.





Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Philip Mpango (watatu katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa mpango wa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha, uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadau wailillia serikali mtaala elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa elimu nchini wamehoji walimu kutoshirikishwa katika mchakato wa kuandaa Mtaala wa Elimu wa Mwaka 2016.

Wakichangia katika mada iliyohusu mtazamo wa walimu kuhusu mtaala huo, wadau hao walihoji sababu za kutoshirikishwa kwa walimu kabla serikali kuupeleka mtaala huo shuleni.

Wadau hao walikuwa katika mkutano wa siku tatu ulioandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (Ten/Met) kwajili ya kujadili ubora wa elimu nchini.

Akiwasilisha mada hiyo, Mshauri wa Elimu wa HakiElimu, Wildaforce Maina, alisema katika utafiti walioufanya mwaka 2018, wamebaini walimu wengi hawana uelewa kuhusiana na mtaala huo.

"Nilifanya utafiti wangu mwaka 2018 na nilichogundua ni kwamba walimu wengi hawana uelewa kuhusiana na mtaala wa mwaka 2016, wengi wameukuta wakati wa kufundisha tu, hawajui ukoje, hivyo wamekuwa wakifundisha tu bora liende," alidai.

Mshauri huyo wa elimu alisema serikali inapaswa kushirikisha walimu pindi kunapokuwa na mabadiliko ya mitaala ili iwe rahisi kujua vikwazo vinavyowakabili.

Meneja Programu wa Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi Tanzania (Tapie), Laurent Gama, alidai mtaala huo ulitangulia darasani kabla ya walimu hawajajua unataka nini.

"Rai yangu, mabadiliko lazima yaendane na mahitaji, lazima kuwe na vifaa vya utekelezaji, vifaa visichelewe kama ambayo mtaala unataka, lazima kuwe na usimamizi mzuri, lazima kuwe na vitabu, lakini ni lazima walimu wapate mafunzo," alisema.

Mtaalamu wa Elimu kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Peter Mlimahadala, alisema walimu kutoijua mitaala mapema ina athari kubwa kwa taifa kwa kuwa wanafunzi wanaozalishwa wanakuwa hawana ubora unaotakiwa.

"Walimu wao ndiyo wanaweza kueleza vikwazo kwa sababu ndiyo wanaofundisha, ndiyo wanatakiwa kutoa ushauri tunatakiwa tufundishaje, hili ni muhimu sana kwa taifa letu, baadaye tutakuwa na wataalamu ambao ni jina tu," alisema.

# Bilioni 600/- kuokolewa ununuzi mafuta alizeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo la Uholanzi (SNV) na Chama cha Wakulima wa Alizeti nchini (Sufa), wako katika mkakati wa kuanzisha jukwaa la wadau wa alizeti ili kuokoa Sh. bilioni 600 ambazo hutumika kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi kila mwaka.

Imeelezwa kuwa jukwaa hilo pia litasaidia kutatua matatizo yanayowakabili wakulima wa zao hilo, hususani upatikanaji wa mbegu bora.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika mkutano wa kujadili kuanzishwa kwa jukwaa hilo, Meneja Mradi wa Agricultural Transforming Market, Ole Sikala, alisema litasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima kujadili matatizo mbalimbali na kuyatafutia utatuzi.

Alisema SNV wako kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wa zao hilo wanafuata sheria na kanuni ambazo zimewekwa na serikali.

"SNV tunasimamia katika maeneo mawili ya kilimo pamoja na mikopo kwa wanawake na vijana," Ole Sikala alisema.

Aliongeza kuwa wanaamini kupitia jukwaa hilo, wakulima wengi hasa wale wa chini, watapata nafasi ya kutoa maoni yao kuhusiana na nini kifanyike ili kusonga mbele katika zao hilo.

Meneja wa Sufa, Stephene Henry, alibainisha kuwa mwaka 2017/2018, Tanzania ilizalisha tani 352,908 za alizeti, akieleza kuwa wakizalisha kwa tija, upo uwezekano wa kupata mafuta ya kujitosheleza kwa mahitaji ya ndani na ziada ya soko la nje.

Alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 700,000 wakati hali ya uzalishaji wa ndani tani 210,000 kwa takwimu za mwaka mwaka 2018.

Vilevile, alisema takwimu zinaonyesha asilimia 60 ya mafuta yanayotumika nchini, yanaagizwa nje, jambo ambalo alisisitiza kuwa halikubaliki.

"Tunapswa kuondoa hii hali ya kuagiza mafuta nje badala yake yapatikane ndani," alishauri.

# Kiwango uchangiaji WCF chawashtua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME wa Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC), imeishauri serikali kupunguza kiwango cha uchangiaji kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa shule zao kutoka asilimia moja hadi 0.5 ili kuleta ulinganifu.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Huduma za Elimu wa tume hiyo, Petro Masatu, katika mkutano wa pili wa walimu wakuu wa shule za awali na msingi zinazomilikiwa na makanisa nchini.

Alisema kiwango hicho kipo juu kwao na kushauri kilingane na cha serikali cha asilimia 0.5 kwa kuwa wanatoa huduma kwa jamii na siyo biashara.

"Baadhi ya dayosisi, shule zinatoa nafasi ya ufadhili kwa watoto wanaotoka familia duni, pamoja na juhudi kubwa inayofanywa, zipo changamoto (akimaanisha matatizo) ambazo tunaomba zitatuliwe, shule kudaiwa leseni za biashara wakati huduma itolewayo na makanisa kwa elimu ni ya hisani, na hili la WCF," alilalama.

Masatu alisema tume pia imeanzisha mitihani ya pamoja kwa wanafunzi wenye mitihani ya kitaifa kabla ya kufanya mtihani wa taifa ili kufanya ulinganifu wa mitihani hiyo. "Tume imeanzisha mitihani ya pamoja katika ngazi ya kanda kwa madarasa ya mitihani ya kitaifa kabla ya mtihani wa taifa kuanza ili kuyaboresha maeneo dhaifu na jambo hili limeanza kutekelezwa," alisema.


Akifungua mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu na Utawala, Dk. George Jidamva, alisema shule za kanisa ndiyo zimekuwa kimbilio kutokana na ufaulu mkubwa.

"Serikali inatambua jitihada zote zinazofanywa na kanisa na taasisi zake katika kujenga elimu ya Tanzania, tusingependa sana wadau wetu wanaosaidia kuelimisha mkawa mnanung'unika," alisema.

Aliwashauri kuwasilisha serikalini matatizo yanayowakumba ili kuangalia namna ya kuzihusisha wizara zinazolengwa kuyatafutia ufumbuzi.

"Kuhusu leseni, ni utaratibu wa kawaida wa serikali kwa mtu yeyote anayefanya shughuli za kujiingizia kipato, napenda hilo tulipate kwa upana wake, tunakwazika na nini linapokuja suala la leseni? Tutaangalia namna ya kulifikisha kwenye mamlaka husika.

"Hili la asilimia moja ya WCF ni mambo ya kukubaliana, yanahitaji mazungumzo ya pamoja ni namna gani hiyo WCF inaweza kulingana na serikali, ni mambo gani kanisa litapoteza au kunufaika, liandikwe kwa lugha ya kitaalamu ili lipitishwe kwa wataalamu wetu washauri mamlaka husika," alisema.





Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (kulia), akiongozana na Mkuu wa Chuo Kikuu cha AL- Sumait kilichopo Chukwani, Rais Mstaafu Amani Abedi Karume, wakati wa mahafali ya chuo hicho juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Azaki zampa neno Mufti usimamizi wa mawaidha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASASI za Kiraia (Azaki) zinazopambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, zimeiomba Ofisi ya Mufti Zanzibar kuchukua hatua dhidi ya mawaidha yanayokwenda kinyume cha maadili na kuratibu walimu wa madrasa.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya asasi hizo, Meneja wa Sera na Utetezi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa), Hawra Shamte, alidai baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakitoa mawaidha yanayomkashifu mwanamke.

Alidai yapo mawaidha yanayotolewa na baadhi ya mashekhe yanakwenda kinyume cha maadili na kuchochea vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Alisema wanawake wamekuwa wakikashfiwa na kudharauliwa maumbile yao kupitia mawaidha yanayotolewa misikitini au mengine yakiwa yamerikodiwa.

"Tunataka nyumba za ibada zitumike vizuri kwa ajili ya kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa sababu mashekhe wanasikilizwa na watu wengi," alisema.

Aliiomba Ofisi ya Mufti ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia na kuratibu shughuli za Waislamu, kufuatilia kwa karibu madrasa za Quran na walimu wake.

Alisema usajili wa vyuo vya Quran pia unahitajika kufanyika ikiwamo kuweka sifa za walimu watakaofundisha wanafunzi kwa kuzingatia maadili na tabia njema.

Alidai vyuo vingi havina mwongozo unaofahamika wa ufundishaji kwa wanafunzi kwa sababu hakuna walimu wenye sifa wanaotambuliwa rasmi.

"Tunaiomba Ofisi ya Mufti kufanya usajili wa madrasa zote nchini na kuweka mwongozo wa ufundishaji unaofahamika na kutumika kwa vyuo vingine," alisema.

# Spika ataka ushirikishaji wa watoto

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amesema mafanikio makubwa yatapatikana iwapo watoto watashirikishwa katika mambo yanayowahusu.

Amesema Serikali ya Zanzibar imetia saini mikataba mbalimbali kuhusu haki za watoto, hivyo wakati umefika sasa kuwashirikisha katika mambo yao.

Aliyasema hayo wakati wa mkutano wa wajumbe wa baraza hilo na ujumbe kutoka Shirika la Umoja wa Taifa Linaloshughulikia Masuala ya Watoto (Unicef).

Alisema mikataba mingi imekuwa ikiainisha juu ya wajibu wa watoto na haki zao ili kuwatayarisha kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Naibu Spika huyo alisema watoto wanapaswa kupewa nafasi ya kujadili mambo yao ili kuwajenga katika mtazamo wa kujiamini.

Alisema kwa sasa kuna matatizo mengi yanayowaathiri watoto kwa kukosa fursa ya kusikilizwa na kusikiliza, hivyo wazazi nao wana wajibu wa kuwasikiliza watoto wao.

Alisema katika kufikia malengo ya dunia, ni lazima watoto kuwezeshwa katika mitazamo mbalimbali, hasa kujengewa kujiamini na kupewa ulinzi wakati wote.

Mwakilishi wa Unicef Tanzania, James Gitau, alisema shirika hilo limekuwa na wigo mpana wa kuwasaidia watoto ambao ndiyo taifa la kesho.

Alisema shirika hilo linatambua umuhimu wa kumjenga mtoto katika kupata haki zake za msingi ili naye kutambua wajibu wake ndani ya jamii.

# Ataja suluhisho ukosefu wa ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHUO Kikuu cha AL-Sumait Zanzibar, kimetakiwa kuzidisha mbinu za ufundishaji katika kozi mbalimbali ili kumsaidia mwanafunzi kujiajiri mwenyewe amalizapo masomo yake.

Naibu Waziri wa Elimu, Simai Mohammed Said, alitoa rai hiyo kwa Niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, huko Chukwani wakati wa mahafali ya chuo hicho.

Alisema mbinu bora ya ufundishaji wanafunzi ni kumsaidia uelewa wa kujua namna ya kujiendesha kimaisha na kujipatia maendeleo.

Aliwataka wanafunzi waliomaliza masomo yao wasitosheke na elimu walioipata, bali wajiunge na vyuo vya nje na vya ndani ili kupata maarifa zaidi.

Pia, aliwataka wanafunzi na walimu kuendeleza kufanya utafiti wa hali ya juu ili chuo kiendelee kuwa na hadhi ya kimataifa.

Akizungumzia tatizo la ufinyu wa eneo la chuo hicho, naibu waziri huyo alisema tayari limeshawasilishwa wizara husika ili kupatiwa ufumbuzi.

Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Dk. Amani Abeid Karume, alisema mahitaji ya elimu yanaongezeka siku hadi siku na chuo kinatarajia kutoa udhamini wa masomo ili kuvutia wanafunzi.

"Mpango wa kuanzisha msingi wa kuwasaidia wanafunzi wenye hali ngumu kimaisha, unaandaliwa ili kuwapatia haki ya elimu wanafunzi hao," alisema.

Aliongeza kuwa chuo hicho kimekuwa na hadhi ya kimataifa na kimetimiza malengo kwa kutoa huduma katika nafasi tofauti za kielimu ikiwamo ushauri nasaha, kompyuta, elimu ya sayansi, masomo ya sanaa na teknolojia habari na mawasiliano.

Wanafunzi 364 wamehitimu masomo yao katika ngazi ya cheti, shahada na stashahada chuoni hapo.




**JUX**

Soma UK.15

JUMAMOSI DESEMBA 14, 2019

BT BURUDANI TELE



# SAUTI MPYA AFRIKA 2020

Soma UK.19

## BASI SAWA



# Ray C apongezwa kupasua jipu

UNAWEZA kusema wameechoka! Ndivyo mkongwe wa muziki wa kizazi kipya, Ray C alipojiita akiliamsha dude wiki hii kwa kumwambia Diamond Platnumz kuacha roho mbaya kwa wenzake.

Kauli hiyo ambayo iliungwa mono na baadhi ya mashabiki wake, aliitoa kupitia ukurasa wake wa Istagram akisema anatakiwa kuacha tabia ya kuwapiga madongo wasanii wenzake na kumtaka kuishi nao vizuri.

Baada ya kutoa kauli hiyo, wafuasi wake walionekana kuwa na maoni tofauti huku idadi kubwa wakionekana kumpongeza kwa kusema ukweli.



# Killy, Ali Kiba waja na 'Gubu' mtaani


MWAKA 2019 unamalizika kwa Kings Music kutoa singo nyingine kali kama zawadi kwa mashabiki wake.

Kibao hicho kilichotambulishwa jana 'Gubu' kimeleta pamoja familia ya King, Killy na Alikiba ambao wamekitendea haki kutokana na ladha yake tamu.

Wimbo huo umetengenezwa na Prodyuza Moko na video yake imetayarishwa na Ivan, wakati picha zake zimechukuliwa Lushoto mkoani Tanga.

# GIGGY MONEY

## KIBOKO KWA MWANAWE




MWANAMUZIKI wa Bongo fleva, Giggy Money, amesema hataki mwanawe kupItia maisha yake, badala yake atahakikisha anamsomesha ili kuwa tofauti na yeye.

Amesema binti yake Mayra anataka asome katika shule ambazo hazitamruhusu kufikiria mambo mengine ikiwamo mitandao ya kijamii ili kumuandaa kuwa na mafanikio katika maisha yake.

"Sitaki mwanangu apitie katika maisha kama yangu, nitahakikisha anapata elimu nzuri ambayo huko baadae itamfanya kuishi vizuri zaidi ya mimi mama yake," amesema Giggy Money.

## INSTA-TWITTER





**Usimcheke** mtu anayelia leo kisa wewe una furaha au mambo yako yamekunyookea. Hali hiyo ni ya mpito tu, jua na wewe huwezi kuwa na furaha milele. Ni vema ukatumia furaha uliyonayo kumfariji na kumpa furaha mtu anayepitia kipindi kigumu-**Rayvanny.**



**Kitendo** cha waimbaji wa muziki wa singeli kuuamrisha umati kutembea kuelekea kulia, kushoto, nendeni nyuma, kisha rudini mbele wa watu wakatii maagizo hayo si kitu kidogo.
Ni kitu cha kupongezwa na kinapaswa kuheshimiwa sana. Tusibishane katika hili-**Roma Mkatoliki.**



## Jux asimulia chungu ya penzi

MWANAMUZIKI wa R&B, Juma Jux, amesema mapenzi yanaweza kupungua pale mazoea yanapozidi kwa watu wanaopendana.

Jux ambaye wameachana na mpenzi wake wa siku nyingi, Vanessa Mdee, amesema lazima watu kupitia hatua tatu ya mapenzi ikiwamo raha, mazoea na machungu na hata yeye amekutana na mambo hayo.

"Lazima watu kupitia furaha pale unapoanza mapenzi, mnapozoeana mambo yanakwenda kombo kwa kuibuka migogoro na hatimaye kuvunjika penzi na kusababisha machungu," amesema.



>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

@burudanitele



## ROSE REE YEYE NA KILEVI MBALIMBALI

BAADA ya kupata tuhuma nyingi kutokana na video chafu iliyosambaa mitandaoni, rapa Rose Ree, amesema yeye hatumii kilevi chochote katika maisha yake.

Akijibu swali katika kipindi cha Planet Bongo, msanii huyo amesema kwake iwe bangi au kinywaji chochote chenye kilevi hakikaribii kutokana na kujisikia vibaya.

"Mimi situmii kilevi chochote iwe Bangi au Pombe, kwanza pia nashangaa watu wanaopenda Pombe, Mimi ladha yake tu inanichefua sana siipendi Pombe" Amesema hayo Rosa Ree.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Maisha** hayataki kujikweza na kujiona kuwa wewe ni wa thamani sana kuliko binadamu wengine. Kumbuka kuna wakati mhitimu wa chuo kikuu anaajiriwa na mtu ambaye hakumaliza hata shule ya msingi. Basi usiidharau elimu, lakini thamini sana utu-**Jenifer Kyaka Odama.**



**Wasanii** wenzio wanatafuta riziki wewe unaanza kuwapiga madongo kabla hata ya shughuli. Ina maana hutaki wenzio nao wang'ae? Ni roho mbaya. Umekosea sana. Tabia mbaya. Ishi na wenzio vizuri, watakie kheri hata kama huhusiki na shughuli-**Harmonize.**



**Kutazama** sana si kuona vyema bali kutazama kwa makini-**Nyamayao.**

# Kuumbe!



# UBAGUZI MISS WORLD?

## WAREMBO WALIOZAA KUIPELEKA MAHAKAMANI

HIVI karibuni kumeibuka malalamiko kutoka kwa wadau wa shindano la Mrembo yaani 'Miss World'wakidai yana masharti ya kibaguzi na hayafai katika karne hii ya 21.

Madai hayo yanaambatana na vielelezo kadhaa ambavyo vinaonyesha baadhi ya washindi walinyanyaswa na kunyang'anywa taji baada ya kugundulika wamezaa.

Moja ya sharti linalolalamikiwa ni mrembo anayetaka kushiriki lazima awe hana mototo.

Kulingana na BBC, mrembo Veronika Didusenko mwenye umri wa miaka 24, alishinda taji la mrembo wa Ukraine (Miss Ukraine) mwaka 2018 lakini alinyang'anywa taji hilo pale waandaaji walipogundua kuwa ni mama.

Na sasa Veronika, ambaye ana mtoto mwenye umri wa miaka 5, ameamua kuchukua hatua za kisheria kwa waandaaji wa mashindano hayo kuhusu sheria zao.

''Nataka niwabadilishe, na kuwapa changamoto. Nataka nihakikishe sheria za kushiriki mashindano ya urembo wa dunia zibadilike na zilingane sawa sawa na wakati huu.'' Aliiambia Radio 1 Newsbeat.

Aliongeza ''Nataka niwaweke sawa kutokana kwa maisha ya sasa na kuangalia maisha halisi ya wanake kwa nyanza hizi, na kutambua kuwa wanaweza kufanya kazi na vile vile mambo mengine nje ya kazi.''

Veronika anadai aliamua kushiriki Taji la ''Miss Ukraine'' kukuza kituo chake cha kusaidia watu na alishangaa alipopewa ushindi wa shindano hilo.

Angeenda kuiwakilisha nchi yake katika mashindano ya urembo wa dunia lakini siku nne baadae alinyang'anywa taji hilo.

'' Ilikuwa ni jambo la aibu na la kufedhehesha kwangu,'' amesema.

''Nilijisikia vibaya kwasababu sio mimi peke yangu ninayofanyiwa haya, ni kitu ambacho wanawake wengi duniani wanakabaliana nacho, ambao labda wanataka kushiriki lakini hawaruhusiwi kushiriki kwasababu tu wana watoto.''

Amekubali kuiona sheria hiyo kwenye fomu ya kuomba kushiriki, lakini alishauriwa kushiriki na waandaji hao.

''Kwanini mwanamke akataliwe kushiriki kwasababu tu ni mama? Alihoji na kisha akasema '' Haitii maanani kabisa''

''Kuwa mama haileti madhara yanayomzuia mshiriki kufanya kazi au kuwa mwanamitindo au kufanya kazi zangu.''

Mwenyekiti na mkurugenzi mkuu wa shirika la 'Miss World', Julia Morley, aliulizwa kuhusu sheria hiyo hakupepesa mdomo na alijibu hakuna maana kubadilisha sheria hiyo.

''Unapojaribu shirika la kimataifa likubaliane na wewe, inabidi uangalie kila mtu na wanapiga kura kulingana na yale yaliyoruhusiwa.''

Akaongeza ''Chochote ninacho hisi mimi au unachohisi umoja wa ulaya ni kitu kingine kabisa kulingana na kile sehemu zingine za dunia wanazokubaliana nayo, inabidi waangalie sheria zao za kidini na mambo mengine kadhaa.''

Veronica anawakilishwa na mwanasheria wa kutetea haki za kibinadamu, Ravi Naik, ambaye anadai chini ya sheria ya haki sawa ya mwaka 2010, sheria hiyo ya kuingilia shindano hilo ni ya ubaguzi.

Mashindano ya ulimbwende nchini Tanzania mwaka 2014 yaliingia dosari kama hiyo kwa madai ya udanganyifu wa kuwa na mtoto na hivyo kuvuliwa taji la Tanzania kwa mwaka huo.

Bi Basila Mwanukuzi ambaye aliwahi kuwa Mlimbwende wa Tanzania 1998 na sasa ni muandaaji wa mashindano hayo hakutaka kuzungumzia suala hilo la kuwa kile kilichotokea Ukraine kiliwahi kutokea nchini mwake, "sikuwa kiongozi wakati huo hivyo sijui chochote.Tunafahamu kwamba kila mashindano yanakuwa na sheria na kanuni na taratibu zake ambazo kila mshiriki anatakiwa kuzifuata na katika dunia hii vitu vinasheria zake.'' Amesema Mwanukuzi.

# 'Mabaharia' wa 5 waliotingisha 2019



**Na Adam Fungamwango**

MWAKA 2019 ndiyo huo unakatika, hautorudi tena, na utabaki kwenye vitabu vya historia milele na milele.

Unamalizika kukiwa na mambo mengi yamefanyika ila muda tu ni mchache. Kwenye tasnia ya muziki wa kizazi kipya wapo wasanii ambao mwaka 2018 walifanya vema, mwaka mwaka huu umewakataa na wamechemsha.

Lakini wapo ambao mwaka huu umewakubali na wametoa ngoma ambazo zimebamba kweli kweli hata ukifika kwenye hafla na sherehe mbalimbali, hazitoisha mpaka ngoma hizo zichezwe na zinazingua watu kweli kweli.

Mitaani, kwenye magari na kwenye maduka nako ukipita kila kona utazisikia. Waliofanya vema mwaka huu wako wasanii wa kiume na wa kike. Lakini leo tunaanza na wasanii wanaume.

### Harmonize

Jamaa ni kama mwaka huu ulikuwa wa kwake. Amekimbiza kisawasawa na kujiongezea umaarufu mkubwa. Wapo watu ambao alipotoka na ngoma yake ya kwanza 'Aiyola' miaka minne iliyopita walidhani amebahatisha.

Alitoa ngoma nyingine, lakini hazikuipiku ile ya kwanza. Lakini mwaka huu amekuja kuthibitisha kuwa amekomaa na sasa ni msanii mkubwa na wa kuheshimika.

Miezi sita iliyopita alishtua watu kwa ngoma ya 'Never Give Up' ambayo ilipendwa mno.

Kabla hajakaa sawa atatoa ngoma zingine mfululizo, lakini zilizomuweka 'juu mawinguni' ni 'Uno' na 'Magufuli'.

### Marioo

Ni mmoja wa wasanii waliokuja juu na wanaotishia ufalme wa baadhi ya wasanii wa kizazi kipya.

Mwaka huu amekuwa tishio kama njaa vile kwa kutoa ngoma ambazo zimekuwa zikikubalika kisawasawa na mashabiki wa muziki huo hasa uswahilini.

Ngoma zake kama 'Raha', 'Ya uchungu', 'Inatosha' zimemfanya kuwa msanii wa kutazamwa kwa jicho la tatu.

Kubwa kuliko zote ni ngoma yake ya 'Anyinya' ambayo huko uswazi inaimbwa hata na watoto wadogo.

### Baddest

'Sijui Nikagongee nyagi? Au nikagongee veve? Sijui nikagongee banana?, Au nikagongee yokozuna?'

Kwa muda wa zaidi ya miezi sita sasa wimbo huu umekuwa ukiwachengua watu wengi. Cha ajabu ni kwamba si watoto, wanawake na vijana waliopenda ngoma hii, bali hata watu wazima.

Kwenye mabasi ya kusafiri mikoani ndiyo unaongoza kwa kufariji abiria waosafiri. Msanii huyu ambaye hakuwa na jina kubwa Baddest amekuwa maarufu ghafla kutokana na ngoma hii ambayo bado inazidi kutamba na kushangaza wengi na kuwa mmoja wasanii waliotisha kama tsunami mwaka 2019.

### Rostam

Rostam ni kifupi cha majina ya wasanii wawili. Roma Katoliki na Stamina. Waliamua kuungana na kuunda umoja wao kuimba kwa pamoja. Kwanza wakaanza na ngoma iliyopendwa sana 'Kaolewa'.

Mwaka huu wametesa sana na ngoma moja hivi matata sana walioiita 'Kijiwe Nongwa' ambayo ilileta maneno mengi sana nchini, lakini hayo hayo maneno ndiyo yaliyofanya ngoma hiyo izidi kupendwa.

### Rayvanny

Siku si nyingi iliyopita ametoa ngoma moja kali aliyoiitwa 'Naogopa', lakini mwaka huu ametoa ngoma nyingine kama 'Chuchumaa' na 'Ilove You' ambazo zimezidi kumuweka kwenye chati.

Rayvanny naye pia mwaka huu amekimbiza kweli kweli na anastahili kuwa mmoja wa wasanii ambao wametesa.

# IMETOKEA

# JOHN CENA AMTOKEA GHAFLA MADJOZI

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi kutoka Afrika Kusini, Sho Madjozi, hivi karibuni alimejikuta akipagawa baada ya kufanyiwa sapraizi ya nguvu ya kukutanishwa na mwanamieleka maarufu, john Cena.

Sho ambaye anatamba na kibao chake cha 'John Cena' alikutana na mwanamume huyo nchini Marekani wakati akifanya mahojiano katika kipindi cha Kelly Clarckson show.

Wakati akihojiwa, mwanamuziki huyo alisema pamoja na kutunga wimbo huo, bado hajakutana na John Cina na kwamba aliona fahari pale alipokuta mwanamieleka huyo akiposti picha yake katika mtandao wa Istagram.

Wakati wote Sho hakufikiria kwamba siku moja anaweza kumuona, japokuwa ana shauku hiyo kwa muda mrefu.

"Siwezi kujua kama nitaweza kuonana naye, lakini nampenda labda hilo ndilo naweza kusema," alisema Sho.

Baada ya kufanyiwa mahojiano, Kelly alimuomba Sho aende kuimba wimbo huo, naye bila shida alikwenda mbele na kuanza kuwaimbia watu walioshiriki katika kipindi hicho.

Wakati alipofika katika sehemu ambayo inataja jina la John Cena, ghafla mwanamieleka huyo alitokea na kusababisha msanii huyo kupagawa asiamini kile anachokiona mbele ya macho yake.

Alimkimbilia haraka Kelly na kuhoji kile alichokifanya kwake na kulalamika hawezi kusahau kwa tukio hilo.

Baada ya hapo alirudi kwa John Cena na kumrukia kama vile mwana anapomuona baba yake kwa mara ya kwanza, hakika ilikuwa furaha kubwa kwa mwanamuziki huyo.

Kibao cha John Cena ambacho kimeimbwa kwa lugha ya Kiswahili, kimekuwa maarufu mara kilipotambulishwa baada ya mchezaji huyo wa mieleka kuposti katika akaunti zake za mitandao ya kijamii.

Kutokana na hatua hiyo, wimbo huo umekuwa na wafuasi wengi walioangalia kupitia You Tube na kuwa miongoni mwa single iliyofanya vizuri katika chati za muziki duniani kote.






# Matashtiti
## Mbuzi hajui thamani ya mkia wake

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine binadamu hawezi kujua thamani ya kitu alichonacho hadi pale kitakapokuwa hakipo mikononi mwake. Binadamu anaweza kumiliki kitu cha thamani, lakini kutokana na mazoea ya kuwa nacho, au kukizoea kukiona tu mara kwa mara anakiona cha kawaida tu. Tatizo linaanza pale kinapochukuliwa na mtu mwingine na yeye kuwa hanacho mikononi au kwenye himaya yake. Hapo naanza kuhisi upungufu wa kutokuwa na kitu kile.

Hata kwenye masuala ya mapenzi. Kuna wanaume au wanawake wanaowachukulia poa wapenzi, wachumba au wanandoa wenzao wakati wakiwa pamoja.

Lakini ikitokea bahati mbaya wanapotengana hali inakuwa mbaya. Kula hakuliki, kulala hakulaliki. Muda, gharama zinatumika kumrejesha mwenza wake. Baadhi wanafanikiwa na baadhi hawafanikiwi na kubaki na kidonda kisichopona milele. Hapa tunajifunza kuthamini kile ulichonacho na usikichukulie poa kwa sababu tu umekizoea.

Ndiyo maana waswahili wakaja na msemo wa 'mbuzi hajui thamani ya mkia wake hadi ukatwe.' Nzi wakianza kumfuata, ndipo anapojua kuwa kumbe mkia ulikuwa na thamani kwake, tofauti na mwanzo alipodhani ni usumbufu tu.

Filamu ya 'Matashtiti' inaonyesha kisa kizima cha jambo hili. Imechezwa na wasanii kama Kingwendu, Tin White, Mtanga na wengineo.

Inaanza kuonyesha kuwa Mtanga akiishi vema na mkewe Lightness. Hata hivyo maisha yao ni ya kawaida tu, ya chumba kimoja kule Tandale jijini Dar es Salaam.

Lightness ni mwanamke mwenye muonekano mzuri pamoja na shepu ya kuvutia wanaume wakware. Sifa za kijinga anazopewa Light kuwa yeye ni mzuri na kwa nini anaishi na mwanamume asiye na pesa, akiishi maisha duni, wakati anatakiwa awe anaishi nyumba yenye kiyoyozi na kupata maraha kama yote hivi.

Sauti nzuri za maneno hayo, yanaingia kwenye masikio na ubongo wa Light, hatimaye anaanza kumfanyia visa mumewe na hatimaye kudai talaka yake. Hali inapokuwa mbaya, Mtanga anaamua kutoa talaka.

Dada huyo ambaye alidhani uzuri wake utaweza kumfanya aishi kama malaika, aliondoka na kwenda kwa mashoga zake kuishi kwa muda wakati anatafuta maisha yake.

Mashoga zake hao kazi yao kubwa ilikuwa ni kulala mchana, ikifika usiku wanajiremba na kwenda kwenye kumbi za starehe kutafuta mabwana.

Lightness naye aliingizwa kwenye kazi hiyo. Baada ya muda mfupi akawa mjuzi zaidi kuliko wenzake aliyewakuta. Ikafika wakati akawa anawachukulia hadi mabwana wenzake. Walipogundua walimtimua.

Safari yake ikamfikisha kwenye mikono ya mwanamume mmoja aliyeitwa au kujiita Makaveli. Alikuwa yuko vizuri kimaisha, akamuweka ndani. Kama alifikiria amefika alipopataka kwenye maisha mazuri, alikosea.

Kumbe jamaa alikuwa na mkewe ambaye alikuwa amesafiri kwenda kujiuguza kwao. Mke wa Makaveli alipona na kurejea nyumbani kwake, akakuta ugeni asioutarajia, likazuka songombingo.

Makaveli na mkewe wakamtimua Lightness. Alichanganyikiwa na kuanza kujiingiza kwenye ulevi, tena akinywa pombe haramu ya gongo. Kutoka kwenye kumbi kubwa za starehe na mahoteli hadi sasa kilabuni. Hadhi ilishuka. Inafika siku akababakwa na walevi wenzake na kupata ujauzito usiokuwa na baba.

Hali ilizidi kuwa mbaya, alikaa kwenye jiwe na kufikiri yote aliyoyafanya. Akajikuta akijilaumu kwa kudai talaka kwa mumewe Mtanga. Akatambua umuhimu wa Mtanga baada ya kuanza kupata shida. Kurejea kwake kuomba msamaha hakuweza kwa kudhani hawezi kumsamehe jinsi alivyomfanya, lakini pia akirejea akiwa na mimba.

Alichoamua ni kupita kwa shoga zake kuomba pesa kidogo zitakazotosha nauli ya kumrejesha kijijini kuanza maisha mapya



# SAUTI MPYA AFRIKA 2020

WAKATI wanamuziki kama Davido, Mr Eazi, Wizkid na Burna Boy wameweza kung'ara mwaka 2019, wana kazi kubwa ya kulinda heshima yao hiyo baada ya kujitokeza zao jipya la wasanii linalotishia nafasi zao.

Wasanii hao kutoka Nigeria, wamekuwa alama ya muziki wa Kiafrika kutokana na kazi zao kuwa juu katika kiwango cha kushangaza.

Kutokana na kutoa kazi bora kulimshawishi Beyoncé kuwachagua kushiriki katika albamu yake iliyopata umaarufu iliyotokana na filamu ya Lion King, huku Mr Eazi na Burna Boy wakicheza muziki wao katika tamasha la mwaka la muziki la Coachella mjini California.

Kulingana na BBC, wasanii hao wanakazi kubwa ya kupambana na wanamuziki watano chipukizi ambao wanaweza kushika nafasi zao mwaka 2020.

Sheebah Karungi (Uganda)

Akiwa na mafanikio ya kimuziki katika nchi yake ya Uganda, muziki wa Sheebah sasa unavuka mipaka.

Akiwa na sauti mahiri, Sheebah amekuwa msanii mwenye malengo.

Kuanzia kushirikiana na wasanii wengine wa Kiafrika, mtindo wake wa mavazi unaonyesha jinsi alivyokuwa na kipaji cha kipekee.

Unapomuangalia kwa haraka utagundua ni mwanamke mwenye uwezo mkubwa na anapokua jukwaani, anabadilika na kuwa staa wa nguvu.

Joeboy (Nigeria)

Joeboy alipata umaarufu kwa wimbo wake Baby, ambao ulitazamwa na watu milioni 18 katika kipindi cha miezi tisa kwenye mtandao wa YouTube.

Akiwa na sauti inayotoka moyoni na kujielezea kwa ustadi katika mtindo wa kipekee wa nyimbo zake, mwimbaji huyu wa Nigeria huwasilisha mistari ya nyimbo zake kwa mitindo ya Afrobeats na pop.

Anapata umaarufu haraka kwa nyimbo hizo mbili tu, amepata wafuasi kote Afrika na tayari ameshafanya onyesho la muziki wake nchini Uingereza.

Brian Nadra (Kenya)

Tumekuwa tukimfuatilia Brian Nadra tangu mwaka 2017 alipotoa single yake 'Leo'.

Anaelezea muziki wake kama wenye hadhi ya kitamaduni, ni mwimbaji na mtunzi wa nyimbo kutoka Kenya mwenye sauti ya kuvutia.

Innoss'B (DRC)

Kwa kutumia muziki wa kitamaduni wa Wakongo, Innoss'B ameweza kuleta sauti ya kisasa katika muziki wa kizazi kipya.

Mwaka huu, muimbaji huyu alipasua mawimbi kwa single yake ya Yo Pe - akishirikiana na nyota wa Tanzania Diamond Platnumz.

Katika kipindi cha miezi mitatu, video yake ilitazamwa na watu milioni 14 kwenye mtandao wa You Tube.

Innoss'B ameweza kujumuisha sauti ya muziki maarufu wa Jamhuri ya Congo.

Sho Madjozi (Afrika Kusini)

Hakuna kitakachomsimamisha Sho Madjozi. Mapema mwaka huu , msanii huyu wa hip-hop wa Afrika Kusini, alishinda tuzo ya BET ya Msanii bora mpya.

Utashi wa kile anachokifanya ndiyo inayompa msukumo msanii huyu. Ukisikia nyimbo zake ni wazi utafurahi anachokifanya.

Analeta utofauti flani katika muziki wa Afrika Kusini kutokana na kutumia lugha ya Kiswahili.

Wimbo wake uliopewa jina la mchezaji wa mieleka wa Marekani John Cena unawasisimua wengi.

# Mapenzi yanavyomchemsha Jordyn




JORDYN Woods ameamua kusimama kidete kukanusha uvumi kwamba ana uhusiano wa kimapenzi na Tristan Thompson aliyekuwa mume wa Kloe Kardashian.

Akitumia akaunti yake ya Instagram, Jordyn alikanusha jambo hilo akisema hana uhusiano na mwanamume huyo ambaye alikuwa mume wa dada wa rafiki yake Kylie Jenner.

Katika kipindi kimoja alimjibu maswali kutoka kwa Shon Thurman ambaye alitaka kujua kama kweli ana uhusiano wa kimapenzi na Tristan, lakini halijibu kwa ufupi "Hapana".



## Cindy ateuliwa ubalozi wa heshima

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria, Cindy Okafor, amejikuta akiangukiwa na nyota ya bahati baada ya kuteuliwa ubalozi wa jimbo la Abia.

Cindy amekuza jina lake kutokana na shindano hilo, aliteuliwa ubalozi wa heshima wa jimbo hilo na gavana wa eneo hilo.


Akiwa na furaha, mrembo huyo aliposti picha ikimuonesha akiwa na kiongozi wa jimbo hilo mara baada ya kuteuliwa.

## Rotimi ajizawadia jumba la kifahari

MWANAMUZIKI na mwigizaji, Rotimi, ameungana na nyota wengine wa Nigeria kwa kumiliki mali za gharama kubwa baada ya kufanikiwa kununua jumba la kifahari.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Rotimi, alianika jumba hilo huku akieleza furaha yake ya kununua wakati akifurahia siku yake ya kuzaliwa.

"Ni siku nzuri kwa kujizawadia, nimenunua nyumba katika eneo zuri na nashukuru nimelipa zote," aliandika Rotimi.





## Card B aunganisha Dhana, Nigeria

RAPA kutoka Marekani, Cardi B, ameamua kutuliza joto kwa mashabiki wa muziki wa nchi za Ghana na Nigeria, akisema ugomvi kati yao umetengenezwa na kihalisi wanapendana.

Akizungumzia ziara yake katika nchi hizo aliyofanya hivi karibuni, alisema nchi hizo ambazo ni majirani wanaishi vizuri na hakuna bifu kati ya mashabiki wa pande zote mbili.

Ghana na Nigeria wapo katika vita kali hasa katika mitandao ya kijamii katika Nyanja ya kisiasa, burudani na mambo mengine muhimu yanayowazunguka.

"Sikuona bifu kati ya watu wa Ghana na Nigeria, ukweli ni wa kutengenezwa tu kama ilivyo kwa Wacominica na Wapuerto Ric," amesema Card B.

## Beyonce hataki umbeya

MKALI wa muziki kutoka Marekani, Beyonce, amejitokeza na kujibu taarifa za kuwa yeye ni mjamzito,

Akihojiwa katika Jarida la ELLE toleo la Januari 2020, amewataka watu kuacha kufuatilia mwili wake kwa sababu ni haki yake kuuhifadhi.

"Achaneni na viungo vyangu vya uzazi" alijibu baada ya kuulizwa kama kweli ni mjamzito.



## SAFU



**MIONZI YA SHERIA**

# Fikiria kuanzisha kampuni ya umma

Na John Juma
0716217615

HIZI ni zama za uwekezaji, uwe mdogo au mkubwa ambao pia unaambatana na masuala ya kulipa kodi na kusajili kampuni.

Hivyo ni vyema kujua faida za kuunda kampuni ya umma badala ya ile ya binafsi. Hili ni jambo ambalo ni vizuri kulifahamu hasa unapotaka kujiingiza kwenye ujasiriamali na uwekezaji.

Kampuni ya umma huitwa 'public company kwa Kiingereza, lugha ambayo mara nyingi ndiyo tunayoirejea kwenye kujifunza masuala ya kisheria.

Kampuni hii hutofautishwa na kampuni binafsi au private company lakini zote ni kampuni kwa ajili ya biashara na mara zote hutegemea unahitaji kufanya nini ili ujue ni kampuni ipi inafaa kuiunda.

Unaweza kujiuliza je, kampuni ya umma inaweza kumilikiwa na watu binafsi?

Jawabu ni ndiyo inawezekana. Watu wengi hudhani kwa kuwa jina la kampuni hii ni umma basi hudhani ni kampuni ambazo huundwa na serikali. Neno umma ni limetokana na namna muundo wa kampuni yenyewe ulivyo yumkini halina uhusiano wowote na kampuni za namna hii kumilikiwa na serikali.

Hivyo yafaa ifahamike kuwa hata wewe mtu binafsi mjasiriamali wa kawaida waweza kuunda kampuni ya namna hii pengine kutokana na faida zinazotokana na kampuni ya aina hii.

**KAMPUNI YA UMMA**

Kwanini uunde kampuni ya umma badala ya kampuni binafsi? Pengine ni swali unaloweza kujiuliza. Uhuru wa wanahisa.

Kampuni ya umma inatoa uhuru mkubwa kwa wanahisa. Wakati kampuni binafsi inaruhusu kuwa na wanahisa mwisho idadi yao ni 50 kampuni ya umma haina ukomo wa idadi ya wanahisa.

Hii ina maana waweza kuwa na wanahisa hata Zaidi ya 1000,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha mwisho isipokuwa kuna ukomo wa kiwango cha chini. Kiwango cha chini inakulazimu kuwa na wanahisa kuanzia wawili.

**UHURU WA HISA**

Suala jingine ni uhuru wa kuuza na kununua hisa. Katika kampuni binafsi hakuna uhuru wa kununua na kuuza hisa. Katika kampuni za kundi hili yatatakiwa kabla ya mwanahisa kuuza hisa zake kwa mtu mwingine ni lazima kupata ridhaa ya wanahisa wenzeke. Wakikataa hakuna kuuza.

Lakini pia, hawawezi kumuuzia hisa mtu ambaye wanahisa wengine hawampendi au kumkubali. Yule wanayempenda na kumridhia ndiye huyo muuza hisa anayeweza kumuuzia na si vinginevyo.

Hii ni tofauti na kampuni ya umma kwani mmiliki wa hisa ndiye anayechagua nani amuuzie hisa zake. Hakuna yeyote kati ya wanahisa wenzake anayeweza kumzuia au kumbana kuuza hisa zake wakati wowote anapotaka kufanya hivyo. Kwa maelezo hayo unaweza kuona kuwa katika kampuni binafsi uuzaji na ununuzi wa hisa ni biashara huru inayotokana na maamuzi au ridhaa ya mtu.

**KUTANGAZA HISA**

Uhuru wa kutangaza hisa katika soko la hisa ni jambo jingine katika eneo hili. Katika kampuni binafsi hakuna ruhusa ya kutangaza uuzaji wa hisa katika soko la hisa. Soko la Hisa Tanzania ni moja tu yaani Soko la Hisa Dar es salaam ( DSE).Wakati kampuni ya umma ruhusa iko wazi kuwa unaweza kutangaza hisa zako na watu wanaoona kampuni yako inaweza kufanya kazi na ina mwelekeo mzuri wanaweza kununua hisa na hivyo kampuni kukua na kujiimarisha. Katika kampuni binafsi hilo haliwezekani.

**UTAMBULISHO**

Kwa upande wa jina la kampuni ya umma, sheria inataka kila jina la kampuni ya umma kuishia na neno Public Limited Company(Plc). Itaanza na jina lolote ulilochagua lakini mwisho lazima iishie hivyo.

Mfano KR Public Limited Company Au Kop Public Limited Company.

Ninaamini inawezekana umewahi kuona mitaani neno PLC katika mabango ya kampuni mbalimbali.

Hili humaanisha Public Limited Company na sio hiari kuweka bango hivyo bali ni lazima kwa mujibu wa maelekezo ya kisheria.

Baadhi ya kampuni ya umma hapa Tanzania ni kama benki za CRDB na NMB kwa kutaja ni chache.

Kwa hiyo hata wewe msomaji unaweza kuunda kampuni ya namna hii kwa faida za kisheria zilizotajwa na safu hii na nyingine ambazi zipo.

# Badilisha unavyosherehekea sikukuu mwisho wa mwaka

Na Gaudensia Mngumi

MWAKA mpya unakaribia na kila mmoja anajitahidi kwa kadri awezavyo kufikiria kuhusu kufurahia na kuwa karibu na familia yake wakati wa mapumziko na sikukuu hizo za mwaka. Kila mmoja anatamani kuwa na uwezo wa kufanya siku hizo kufurahisha watoto wake, kama ni Wakristo wanatamani wanafamilia wao wale, kunywa na kuvaa vizuri. Tena wawe na burudani na kuona Krismasi ni mpya na inayovutia, kuliko ilivyokuwa mwaka jana. Aidha, kwa mwaka mpya wengi wanatamani kuona familia zikifurahi na kujisikia tofauti na jinsi sherehe zilivyokuwa mwaka jana au miaka iliyotangulia.



Watoto wakifurahia zawadi za Noeli. **PICHA:MTANDAO.**

**FIKRA MPYA**

Mwaka huu ni vizuri kuanza kusherehekea Krismasi na mwaka mpya katika mambo mengi mapya kuwa mbunifu na si lazima sikukuu zifanane kila wakati.

Fikiria misosi siyo kila mwaka pilau, gundua kitu kingine. Angalia pia hata muundo wa kuweka meza , sahani juu yake, anza kuona jinsi utakavyobadilisha meza na kuongeza kitu ambacho unaweza kula na kila mmoja akakifurahia.

Angalia chakula chenye ladha tofauti ikibidi jaribu biryani , weka samaki wa kuchoma, kula bata badala ya kuku, fikiria nyama ya mbuzi , ng'ombe na hata bata mzinga. Kwa wanaoishi mijini.

Kadhalika kijijini awape nafasi jamaa wa mjini kuandaa kitu tofauti cha kuifurahisha familia ikibidi pika biriyani na pilau ya kuku au bata kama unaweza badala ya nyama ya ng'ombe. Andaa tofauti na ulivyozoea. Ni vyema kuongea na watoto na marafiki kuhusu upishi. Kila mmoja ashiriki apike misosi na madikodiko ya kuvutia siyo kila siku dada wa kazi pamoja na mama ambaye muda mwingi anatoa maelekezo wala hapiki (hasa kwa wakazi wa mijini).

**KUPEANA ZAWADI**

Pengine Watanzania hawapeani zawadi kama wanafamilia. Unaonaje mwaka huu ukiwapa watoto, mama, baba na ndugu wengine zawadi za Krismasi na mwaka mpya? Wape zawadi watoto waliofanya vizuri shuleni, lakini pia wale wanaojituma kufanyakazi nyumbani, mtoto mtiifu atambuliwe, anayelisha mifugo atunzwe, anayelima na kusafisha mazingira, kutunza maua , kuchota maji, kupika kufua ngua na kuwatunza wadogo zake. Bila kujali kuwa uko kijijini angalia mambo mazuri ambayo wanafamilia wanayafanya wape zawadi kama kalamu, soda, biskuti, daftari, dayari, soksi , viatu na shuka kulingana na uwezo wako na uwakumbuke hata wale wanaoamka asubuhi na kuwasha moto.

**KUKUMBUSHANA YA 2019**

Ni vizuri kama familia kukaa na kukumbushana mambo ya mwaka 2019 kila mwanafamilia aseme lilomuudhi, kumfurahisha na kusema anapendelea kitu gani 2020.

Inafaa kuandika mambo hayo na kuwa na wakati wa kujitathimini ikifika mwaka 2021. Kufanya hivyo inawezekana kukawaleta wanafamilia pamoja katika kupanga na kutekeleza miradi ya nyumbani kwenu. Lakini pia kuhamasisha watu kupendana zaidi na kujiona kuwa kila mmoja ana nafasi ya kuboresha na kufurahisha mwenzake kwa vile anajiona ana mchango.

**WAZAZI Vs WATOTO**

Mwaka unavyoelekea ukingoni ni vizuri wazazi na walezi kuwapa watoto nafasi ya kuwatathmini ili kujijua na kurekebisha upungufu uliopo. Kwa mfano waache watoto wasema kama baba au mlezi wa kiume ni mlevi, anachelewa kurudi nyumbani, anamnyanyasa mama na watoto ili kujirekebisha.

**TENGENEZA KUMBUKUMBU**

Ni vizuri sasa watu waanze kuweka kumbukumbu za picha na matukio ya siku za sikukuu za mwisho wa mwaka.

Huenda Watanzania wengi leo hawana picha ya jinsi walivyosherehekea Noeli au siku kuu ya mwaka mpya mwaka 2018. Usipuuze weka kumbukumbu ya 2019 ili uifurahie itakapofika mwisho wa mwaka wa 2020.

Ni vyema kupiga picha simu zipo na wengi wana simu janja ni vizuri kufanya hivyo ili kuweka kumbukumbu. Picha za simu zinaweza kusafishwa na zikawekwa kwenye kitabu cha picha na watu kuendelea kukumbuka miaka inavyokwenda. Ni vyema kutumia teknolojia hiyo ya simu janja ili kuunganisha zaidi familia.

Mama na baba au watoto wanaweza kuchagua picha bora, kuziandika na kuweka albamu ya picha za matukio ya mwaka jana . Yote haya yanaweka taarifa za kizazi zcha sasa na vijavyo.

**IBADA MWAKA MPYA**

Ukubali ukatae ibada ya shukrani ni muhimu. Ni vyema kama familia kukubaliana kuwa ni lazima kama ndugu kuwa pamoja kwenye ibada ya Noeli na mwaka mpya.

Ni vizuri kama familia kushikamana na kushikana mikono, mkasali nyumbani na pia kuingia kanisani au msikitini kumshukuru Mungu kwa ajili ya mwaka mpya.

Ni vyema kukumbuka kama familia kuwa ni vyema kumshukuru Mungu kuendane na kuwasaidia wahitaji kwa kuwapa zawadi iwe chakula, mavazi, viatu, shuka , godoro na chochote ili shukrani hiyo iwe na tija kwa wanadamu na watu wanaokuzunguka.

**REKODI MWAKA MPYA**

Unapoanza mwaka 2020 ni vyema kuanza kuweka rekodi za mambo muhimu ya kifamilia. Usiache mambo yakapita bila kujiwekea kumbukumbu ili uweze kuangalia na kujifunza kutoka kwenye hatua mbalimbali ulizopitia.

Ukinunua shamba andika. Mwanafamilia akisumbuliwa na magonjwa andika , akipona weka kumbukumbu pia.

# Ngono za makahaba zaw

## ■Wanavyouza mazao kununua ngono
## ■Familia zabaki taabani
## ■Wadau, polisi waingilia kati

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KILIMO kina raha zake hasa kipindi mkulima anapovuna mazao, baadhi huyatenga kwa ajili ya chakula na mengine huyauza ili kujipongeza baada ya kuvuja jasho yeye pamoja na familia.

Matumizi yanavyopangwa hutofautiana, wapo wanafunzi wanaohitaji ada, kina mama mavazi na bidhaa za nyumbani kama magodoro, shuka na vyandarua lakini kuna wanaume wanaofurahia pombe na starehe hasa ngono.

Ndiyo maana starehe hizo hasa ngono zimewaibua makahaba, ambao hutoka mjini kinapofika kipindi cha mavuno na kwenda kufanya biashara ya ngono, ili kuchuma fedha za wanaume wa vijijini na hatimaye kuwaachia umaskini.

Moja ya kijiji mkoani Shinyanga ambacho kimekuwa kikikabiliwa na changamoto hiyo ni Butini kilichopo Kata ya Itwangi, Wilaya ya Shinyanga.

Huko baadhi ya wanaume wamekuwa wakinunua ngono kwa makahaba hao kutokana na fedha za mazao bila kujali kuwa ngono hizo huwaachia maradhi, umaskini na athari za kisaikolojia.

Peter Shilinde, mwanakijiji hicho cha Butini anasema alikuwa ni miongoni mwa wanaume ambao walikuwa wakiuza mazao na kwenda kununua ngono kutoka kwa makahaba hao wa mjini.

Anasema matokeo ya starehe hiyo ni kubakia maskini na anajutia kufanya kitendo hicho ambacho kilimfanya kuwa fukara aliyechezea nguvu zake.

**MAMBO YALIVYOKUWA**

Shilinde anasimulia kuwa kipindi hicho alikuwa mlevi sana na mke wake ndiye aliyekuwa akienda shambani kulima pamoja na watoto, lakini linapofika msimu wa mavuno yeye ndiye mwamuzi wa kwenda kuuza, na anapopata fedha huitelekeza familia yake na kwenda kununua ngono kwa makahaba hao.

Anasema familia yake ilikuwa ikilima hekari tatu za mpunga na mauzo yote aliyamalizia kwenye ngono.

"Ni watafutaji kweli walikuwa wakihitaji kuanzia Sh. 80,000 hadi 100,000, ndipo wafanye mapenzi, na kama hawana fedha hizo watoe gunia moja la mpunga.

"Hapa kijijini kwetu kuna ujinga huo, wanaume kuuza mazao yao ili kwenda kununua ngono kwa makahaba wa mjini, ambao hufika hapa kwa ajili ya kufanya biashara ya kuuza miili yao na mimi nilikuwa ni miongoni mwa wateja wao. Lakini nimeacha baada ya kuona naendelea kuwa maskini, duni na mjinga," anasema Shilinde.

Anasema kuwa aliponunua ngono aliinyanyasa sana familia yake na alikuwa anauza mazao yote na kwenda kuwahonga watu hao waliokuwa wajasiriamali wa mapenzi.

"Nilikuwa maskini wa kutupwa naishi kwenye nyumba ya nyasi, lakini baada ya kuacha sasa hivi nimejenga nyumba ya kisasa ya bati,"anaongeza Shilinde.



Peter Shilinde mkazi wa kijiji cha Butin akizungumza na wananchi.

**KILIO CHA KINAMAMA**

Mkulima huyu anasema bado kuna baadhi ya wanaume ambao walikuwa wakinunua pamoja naye wanaendeleza tabia hiyo, na kuiomba serikali pamoja na mashirika yatoe elimu kwa wanaume ili waachane na mienendo hiyo inayotesa wanawake na familia.

Teresia Kazilo ni miongoni mwa wanawake wakazi wa kijiji hicho cha Butini, anayesimulia namna mumewe alivyokuwa akiuza mazao yote na kwenda kununua makahaba wa mjini maarufu kama makahaba wa Sentani ambalo ni eneo biashara ya ngono hufanyika, na hatimaye kuiacha familia bila ya chakula.

Anasema alipokuwa akijaribu kumzuia alikuwa akimpiga mno na ili kuondokana na usumbufu aliouita kero ya mkewe alitoweka nyumbani na fedha za mauzo ya mazao na kuishia kusikojulikana kwa siku kadhaa na akirudi fedha yote imekwisha na kukimbilia kuuza mazao mengine hadi yanapoisha ndani na kurejea kuishi kwenye umaskini, njaa na magonjwa kwa vile hakuna hata senti ya kwenda hospitalini.



Tereza Kazilo, akielezea masahibu yaliyompata.

"Chakula kinapoisha ndani, nilikuwa na lazimika kwenda kutafuta vibarua kwa matajiri ili nipate fedha ya kuhudumia watoto wangu wasife na njaa, kwa sababu baba yao ni mlevi na hajali familia,"anasema Kazilo.

"Nashukuru Mungu shirika moja la Kivulini lilifika hapa kijijini na kutoa elimu ya kupinga masuala haya ya ukatili, ndipo mume wangu akabadilika na sasa hivi tumejenga nyumba ya bati yenye vyumba viwili ameacha kuuza mazao kwenda kununua ngono kwa makahaba,"anaongeza.

**VIONGOZI WA KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Butini, Masanja Ikingo, anakiri baadhi ya wanaume kijiji humo kuuza mazao yao na kwenda kununua makahaba na kubainisha wamekuwa wakitoa elimu kwa wanaume kuacha tabia hiyo kwani imewafilisi wengi lakini baadhi yao wamebadilika na wengine wanaendeleza .

**BIASHARA IKOJE?**

Ikingo anasema tabia hiyo imekuwa ikijitokeza sana kwenye msimu wa mavuno, ambapo kuna ongezeko wa 'wadada poa' wengi kutoka mjini wakiingia kijijini humo kwa njia ya kufanya biashara ya kuuza pombe ama kununua mpunga, lakini kumbe kazi yao kubwa ni kufanyabiashara ya kuuza ngono.

"Tumekuwa tukitoa elimu sana kwa wanaume kupitia mikutano ya hadhara pamoja na vikao vyetu ya sungusungu, kuwaonya kununua makahaba hao lakini muitikio wake siyo mzuri, kwa sababu baadhi yao bado wamezama na wanapoteza fedha na heshima kwenye familia kwa kununua ngono" anasema Ikingo.

Anasema baada ya kuona hali siyo nzuri kwa wananchi kuendelea kuwa maskini, ikawabidi kudhibiti ukakahaba, lakini ikashindikana kwa sababu wanakuja na vibali vya kufanya biashara ya kuuza pombe na kununua mazao, hivyo ukakosekana ushahidi wa kuwabana, na hivyo kuendelea na biashara zao ni msimu wa mavuno ukiisha wanaondoka.

Claudi Kimaro ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Itwangi, anasema makahaba hao huingia vijijini humo kwa kujifanya wafanyabiashara ama wanunuzi wa mpunga wanaokwenda kwenye makundi na kupanga vyumba vijijini.



Ofisa wa Jeshi la Polisi kutoka dawati la jinsia mkoani Shinyanga, Victoria Maro, akitaja takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watu wazima mkoani humo, kwa mwaka huu kuwa wamepokea kesi 368.

MAKALA

# azengua wakulima vijijini



Ofisa Tathmini na ufuatiliaji kutoka Shirika la Kivulini, Godfley Paschal, akitoa elimu kwa wanavijiji .

Anasema mradi huo ulianza mwaka 2017 na utakoma mwaka 2021, ambapo wanautekeleza kwa awamu kwa kila mwaka, ambapo kwenye utekelezaji wa mradi huo changamoto kubwa ambayo wanakutana nayo ni wanaume kuwafanyia wake zao ukatili wa kiuchumi, wa kuuza mazao na kuhonga makahaba ili kununua ngono.

Anasema kijiji hicho cha Butini kilichopo ni miongoni mwa vijijini vingi kwenye halmashauri hiyo, ambavyo huvamiwa na 'madada poa' kutoka mjini wakati wa msimu wa mavuno, ili kufanya biashara ya ngono na kuchuma fedha za mauzo ya mavuno kutoka kwa wanaume na kuwacha kubaki maskini.

"Shirika la Kivulini hutoa elimu kwa wananchi ya kupinga matukio ya ukatili, pamoja na kuwapatia wanaume elimu ya kujitambua na kuacha kuzifanyia familia zao ukatili wa kiuchumi, kwani baadhi yao wameshaacha na wamekuwa watoaji wa ushuhuda wazuri sana,"anasema Paschal.

"Lakini hatukuishia tu kutoa elimu, bali ilibidi tuunde kikundi cha wanamabadiliko kutoka kwenye kata zote tatu ambazo tunatekeleza mradi wetu, ambao tumewapatia mafunzo mbalimbali ya kupinga matukio ya ukatili, na namna ya kutoa msaada wa kisheria kwa mtu ambaye amefanyiwa ukatili ukiwamo wa kiuchumi,"anaongeza.

**KESI 368 POLISI**

Victoria Maro ni Ofisa wa Jeshi la Polisi kutoka dawati la jinsia mkoani Shinyanga, anataja takwimu za kesi ambazo wamezipokea mwaka huu za unyanyasaji wa kijinsia kwa watu wazima, kwa mkoa mzima wa Shinyanga zimefikia 368.

Aidha, amezichanganua kwa kila halmashauri, Ushetu wamepokea kesi 57, Msalala 68, Kishapu ni 26 wakati Kahama 155 na Shinyanga 62 .

Anabainisha kuwa kati ya kesi hizo 368, zilishoisha na kutolewa hukumu ni 108, zilizotajwa mahakamani ni 109 na mbazo zipo kwenye upelelezi ni 114.

"Kinadada hawa wanakuja na vijijini wakiwa na masanduku ya bia na kujifanya wafanafanya biashara lakini wanauza ngono na msimu wa mavuno ukiisha wengine huondoka na magunia ya mpunga, na kubaki tukijiuliza wametoa wapi na kukosa majibu," anasema Kimaro.

**KUTUNGIWA SHERIA**

Kimaro anasema za mwizi 40, wamejua dawa ya kuwakomesha: "Lakini niseme inatosha. Katika msimu wa mavuno wa mazao mwakani 2020 tumejipanga kuwabana makahaba hawa, kwa kutunga sheria ndogo za vijiji, kuzuia uzururaji wa usiku na unywaji wa pombe nyakati hizo, pamoja na kufanya doria kwenye vyumba ambavyo hupanga makahaba hao, ili kudhibiti biashara hiyo ya ngono," anaongeza Kimario.

Diwani wa viti maalumu wa kata hiyo ya Itwangi, Mengi Zengo, anakiri baadhi ya wanaume vijijini kuuza mazao yao na kununua makahaba hao wa mjini, huku akiwataja hadharani wanaume ambao huendekeza tabia hiyo na kuwaonya waache mara moja kwani wataendelea kuwa maskini.

Anasema kuna baadhi ya wanaume anawafahamu ambao wamekuwa wakinyanyasa familia zao na kwenda kununua makahaba hao wa mjini, huku akiwapongeza wale ambao wamebadilika na kuachana na vitendo hivyo, ambavyo vilikuwa vikididimiza uchumi wa familia zao.

Mwenyekiti wa Halmashuari ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, analaani tabia hiyo ya wanaume kuuza mazao yao na kwenda kununua ngono na kutajirisha makahaba, na kuwataka wabadilike na wajikite kufanya maendeleo katika familia zao.

Anasema elimu ambayo wanapewa ya kutokomeza matukio ya ukatili, waitekeleze kwa vitendo ili kuja kujenga kizazi salama, na siyo kuzalisha familia ambazo hazina maadili na hatimaye kuliharibu taifa kwa kuwa na kizazi kichafu.

"Nawaomba sana watendaji wa serikali pamoja na mashirika mbalimbali mwendelee kutoa elimu ndani ya jamii, ili kutokomeza vitendo hivi vya ukatili, ambapo wananchi hawa kinachowasumbua ni ukosefu tu wa elimu ya kujitambua. Lakini wakielewa vizuri tabia hizi zinazorudisha nyuma maendeleo zitakwisha,"anasema Mboje.

**WADAU**

Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji kutoka Shirika la Kivulini ambao wanatetea haki za wanawake na watoto, Godffrey Paschal, anasema katika halmashauri hiyo wanatekeleza mradi wa kupinga vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia kwenye kata tatu ambazo ni Nyida, Nsalala, pamoja na Itwangi.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mbonje, akiwataka wanaume kuacha kuendekeza matukio ya ukatili ndani ya familia zao. **PICHA ZOTE: MARKO MADUHU**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 24 00)



Dondoo: Kulia
1. Mnyama mwenye singa
4. Jeruhiwa
9. Jina la zamani la Malawi
10.hekima
11.adabu, staha
13.Ng'ata
14.Kitu kitolewacho kudhamini
16.Idadi ya amri za Mungu
17.Nchi ya asili ya sultani
20.Kera
23.Sebule
26.Uchukuaji wa kilichopotea
27.Lokesheni
28.Mmea wenye ncha kali
29.Mwezi wa nane
30.Msalani

Dondoo: Chini
1. Tetesi
2. Kigali ni mji wake mkuu
3. Kiongozi wa jadi wa Wazulu
5. Mamlaka
6. Elemewa
7. Elezwa
8. jambo linalofanywa tena
12.kiongozi wa sala msikitini
15.Makazi ya binadamu
18.Mtu anayetumikishwa
19.Baghala
20.Zana ya kupasulia kuni
21.Mwana
22.Karo ya shule
24.Kata
25.Ulikuwa mji mkuu Romania

## Jibu toleo lililopita



# Wanawake Musoma walivyoamka, wang'ara kuchangamkia mikopo

**Na Sabato Kasika**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo, akizungumza kabla ya kukabidhi hundi kwa vikundi mbalimbali.

KUWAWEZESHA wanawake ili washiriki kwenye uwekezaji wa aina mbalimbali na kuchangamkia fursa za kiuchumi ndani na nje ya jamii zao ni jambo linalosisitizwa na serikali, ambayo imetoa maelekezo ya kufikia azma hiyo.

Kwa hiyo, kila halmashauri inaelekezwa kutenga kutoka katika mapato yake ya ndani asilimia 10 ya fedha kwa ajili ya kukopesha mikopo isiyo na riba vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Wilayani Musoma, wanawake na makundi mengi hayako nyuma, hivi karibuni vikundi 23 vya wanawake, vijana na walemavu vimejitokeza kuomba mkopo usio na riba wenye thamani ya Sh. milioni 116.5.

Katika makabidhiano yaliyofanyika hivi karibuni na Nipashe kuhudhuria hafla hiyo, vikundi vyenye wanachama 408, vilinufaika na mikopo hiyo.

Katika makabidhiano hayo yaliyofanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo, kwenye makao makuu yaliyoko Mugango, wanawake, vijana na wenye ulemavu walionyesha jinsi walivyodhamiria kubadili maisha yao.

Kwa mujibu wa Kayombo, wanawake wamejitokeza kwa wingi kuchangamkia mikopo hiyo wakiwa ni vikundi 16 ambavyo vimekopeshwa jumla ya Sh.milioni 80.5, huku vijana wakipata Sh. milioni 21.

"Vijana walikuwa ni vikundi vinne vyenye wanachama 78, ambao wamepewa kiasi hicho cha fedha na kufuatiwa na walemavu vikundi vitatu vyenye wanachama 45 na wamepokea Sh. milioni 15," anasema.

Vikundi vya wanawake vinatoka katika vijiji vya Murangi, Tegeruka, Kwikuba, Bukima, Bujaga, Saragana, Kwibara, Kataryo, Bwai Kwitururu, Busungu, Mayani na Kome kwa mujibu wa Kayombo

"Vikundi vya vijana vinatoka katika vijiji vya Lyasembe, Maneke, Kataryo na Kisiwa cha Rukuba wakati vya walemavu vinatoka vijiji vya Bukima, Murangi na Nyambono," anasema Kayombo.

Mkurugenzi huyo anasema, utoaji wa mikopo isiyo na riba ni endelevu, na kwamba vipo vikundi vilivyopewa mikopo mwaka wa fedha wa 2018/2019 na vingine bado vitapewa ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2019/2020.

**UTOAJI ENDELEVU**

Kayombo anasema, sasa ni mara ya tano kwa mwaka huu halmashauri yake ikitoa mikopo, na kwamba kwa mara ya mwisho ilitoa Sh. milioni 101 Juni mwaka huu kwa vikundi 25 ikiwa ni sawa na asilimia 92.6 ya mkopo.

"Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri ya Sh. bilioni 1.09, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ndiyo ambayo tumetenga asilimia 10 ya mapato hayo kwa ajili ya mikopo ya wanawake, walemavu na vijana," anasema.

Anasema, mwezi huu, halmashauri yake imetoa mkopo tena kwa vikundi vingine 23, ambavyo vimekabidhiwa jumla ya Sh. milioni 116.5 huku akisisitiza mikopo itumike kwa kile kilichokusudiwa.

"Kwa kuwajali na kuwapenda wanyonge, serikali ya awamu ya tano ya Rais John Magufuli, imeondoa riba kwenye mikopo ya vikundi, sasa hivi pesa utakayokopa ndiyo utakayorudisha," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, wakopaji wanatakiwa kurejeresha mikopo kwa wakati ili kuepukana na ucheleweshaji, ambao unaweza kusababisha kupigwa faini ya asilimia 10 ya kile walichokopa.

**ZAWADI YA KRISMASI**

Katika shughuli ya utoaji mikopo hiyo, mgeni rasmi alikuwa mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo na aliahidi kutoa majembe ya kukokotwa na ng'ombe (plau), kwa vikundi vinavyojishughulisha na kilimo.

"Ninatarajia kutoa zawadi hiyo ya plau Jumanne ijayo Desemba 24 huu kwa baadhi ya vikundi vinavyojishughulisha na kilimo ikiwa ni juhudi za kuendelea kuongeza uzalishaji wa mazao," Prof. Muhongo anasema.

Profesa Muhongo anasema, kwa kutumia kaulimbiu ya maendeleo kwa vitendo anashirikana na wananchi kuanzisha vikundi mbalimbali ambavyo vinajishughulisha na kilimo cha mboga cha umwagiliaji.

Mbunge huyo anasema, aliviwezesha kwa kuvipa vifaa mbalimbali zikiwamo pampu za umwagiliaji, na sasa anajiandaa kutoa zawadi ya plau kwa baadhi ya vikundi, ili viweze kupiga hatua.

**WALIONUFAIKA**

Kiongozi wa kikundi cha wanawake cha Umoja, kilichopo kijiji cha Bukima, Loyce Mugini, anasema wao wamekopa Sh. milioni 10 ambazo watazitumia kuongeza vifaa hasa viti, meza na maturubai ili kuimarisha mradi wao.

"Mradi wetu ni wa kukodisha vitu, kwenye shughuli mbalimbali zikiwamo sherehe na misiba, hivyo tunataka tuongeze, viti, maturubai, sahani na vitu vingine vya muhimu kwa ajili ya mradi wetu," anasema Loyce.

Kiongozi wa vijana wa kikundi cha Pamoja Tunaweza, Aussy Kambi, cha kijiji cha Maneke, anasema kikundi chao kimepata Sh. milioni nne ili kukodisha mashamba na kununua pembejeo, kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

"Sisi tunajishughulisha na kilimo bustani, lakini sasa tunataka kujikita kwenye kilimo cha mpunga baada ya kukumbana na changamoto nyingi kwenye kilimo cha awali," anasema Kambi.

Kambi anasema, kikundi chake kinaundwa na vijana 14, ambao wameamua kuendesha maisha kwa njia ya kilimo badala ya kushinda vijiweni kana kwamba hakuna shughuli za kufanya.

"Tumekopa kiasi hicho cha fedha na tunatakiwa kurejesha Sh.333, 333 kila kila mwezi, na ndani ya mwaka mmoja tunakiwa tumemaliza kutejesha mkopo tulioomba," anassema.

Kwa upande wake katibu wa kikundi cha wenye ulemavu cha Tujikomboe cha kijiji cha Bukima, Jonathan Majura, anasema, waliomba mkopo wa Sh. 9,000,000 lakini wakapata Sh. milioni tano.

"Tumepewa kiasi hicho na tutakitumia katika shughuli zetu za ufugaji wa kuku wa kienyeji, bustani na kukopeshana kwa riba, lakini tukihakikisha kwamba tunarejesha mkopo kwa wakati," anasema Jonathan.

Katibu huyo anasema, kikundi chao kina wanachama 13, huku wake wakiwa ni watatu na wanatarajia kuongeza wanachama wengine zaidi watakapofanya mkutano wao wa mwaka mwezi huu.



Wanachama wa vikundi wakiwa ukumbini kabla ya kukabidhiwa hundi.
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

HABARI KIMATAIFA

# Haftar atangaza ‘vita vya mwisho’ Tripoli

**TRIPOLI,** Libya

KAMANDA wa vikosi vinavyodhibiti sehemu ya mashariki ya Libya, Khalifa Haftar ametangaza alichokiita, ‘‘vita vya mwisho’’ vya kuukamata mji mkuu wa nchi hiyo, Tripoli, kutoka serikali inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa (UN).

Kauli hiyo ya vita ameitoa Haftar (pichani) akivalia nguo za kijeshi, katika kituo cha televisheni cha Hadath cha nchini Libya.

‘‘Leo tunatangaza vita vikali vya kusonga mbele kuelekea kwenye kitovu cha Tripoli na kuukomboa mji huo, ili kuvunja minyororo na kuwaachia huru mateka wake, na kueneza furaha katika mioyo ya wakazi wake.’’

Alisema mbabe huyo wa kivita, na kuongeza kuwa ‘‘Tripoli itarejeshewa nuru yake ya kihistoria, na kuwa tena mji mkuu wa utamaduni.’’

Khalifa Haftar alisema imewadia saa ya operesheni kali, ambayo alidai kila mtu huru na mwenye heshima yake nchini Libya alikuwa akiisubiri kwa shauku kubwa.

Alitamba kuwa vikosi anavyoviongoza vya Jeshi la Taifa la Libya-LNA vitapata ushindi katika vita vya kuikomboa Tripoli, ambayo amedai imegeuzwa kuwa ‘‘pango la wahalifu, ambamo watu hunyanyaswa kwa mtutu wa bunduki’’

Muda mfupi baada ya tangazo hilo la vita, chombo cha habari cha vikosi vyake kimesema vikosi hivyo vimechukua udhibiti wa chuo cha kijeshi kusini mashariki mwa Tripoli katika mkoa wa Salah Eddin. Chombo hicho pia kimearifu kuwa mkoa mwingine wa Al-Tougar umeanguka mikononi mwa vikosi vitiifu kwa kamanda Khalifa Haftar.

Katika tangazo lake Haftar ameahidi kuwapa njia salama wapiganaji wa mjini Tripoli ikiwa watakubali kuweka chini silaha zao na amevitaka vikosi vyake kuheshimu nyumba za wananchi.


Kwa upande mwingine, serikali ya Libya inayotambuliwa kimataifa imesema inadhibiti hali ya mambo mjini Tripoli, na kwamba jeshi lake lilikuwa likifanya doria katika maeneo ya Kusini mwa mji huo.

Waziri wa Mambo ya Ndani Fathi Bashagha, alisema wako tayari kurudisha nyuma kile alichokiita, ‘‘jaribio lolote la kiwenda wazimu kutoka kwa mbabe Haftar.’’

Aprili mwaka huu, Khalifa Haftar, aliamuru kampeni ya kijeshi ya kuukamata mji wa Tripoli kutoka serikali ya Waziri Mkuu Fayez al-Sarraj, lakini kwa wakati huu mgogoro huo ulikuwa katika hali ya mkwamo.

Libya imekuwa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe tangu kuangushwa kwa utawala wa muda mrefu wa Muamar Gaddafi mwaka 2011.

DW





Waziri Mkuu akishangilia ushindi. **PICHA: DW**

# Chama tawala Uingereza chashinda kwa kishindo

**LONDON**,Uingereza

CHAMA cha kihafidhina cha Waziri Mkuu Boris Johnson kimeshinda kwa wingi mkubwa wa kura kwenye uchaguzi mkuu wa Uingereza.

Umoja wa Ulaya (EU) umetoa pongezi nyingi kwa kuhimiza mchakato wa kujitoa katika EU uidhinishwe haraka.

“Serikali ya kihafidhina ya nchi hii imepatiwa madaraka makubwa zaidi ya kukamilisha mchakato wa Brexit. Na si tu kukamilisha mchakato wa Brexit bali pia kuiunganisha nchi yetu na kutanguliza mbele mahitaji muhimu ya Waingereza.”

Alisema Waziri Mkuu Boris Johnson, mara baada ya kuthibitika ushindi wa chama chake cha kihafidhina.

Johnson alipania na anasema kuitoa Uingereza katika Umoja wa Ulaya hadi ifikapo January 31 mwaka 2020 ni kazi itakayofanyika.

Aliwashukuru wote wale waliokipigia kura chama chake. Kwa mara ya kwanza chama cha kihafidhina kujipatia wingi mkubwa wa viti bungeni.

“Mmetupatia kura zenu bila ya kujali kuwa nyie si wahafidhina,” alisema Waziri Mkuu Johnson baada ya idadi isiyo ndogo ya wafuasi wa chama cha upinzani cha Labour kukipigia kura chama hicho cha kihafidhina.

Mwenyekiti wa chama hicho cha upinzani, Jeremy Corbyn, alisema hatagombea tena wadhifa huo kufuatia pigo la uchaguzi mkuu wa jana.

Wakati huohuo, pongezi kwa ushindi wa chama cha kihafidhina zimetumwa na viongozi kadhaa wa dunia.

Rais wa Marekani Donald Trump, alisema katika salam zake za pongezi za ushindi wa Johnson unamaanisha Uingereza na Marekani zitakuwa huru “kufikia makubaliano mapya ya biashara baada ya Brexit.”

Viongozi wa EU wameupongeza pia ushindi wa Boris Johnnson na kutoa wito wa kupigiwa kura haraka na bunge la nchi hiyo mchakato wa kujitoa Uingereza katika EU.

Hata hivyo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Cheki anaonya kuwa ushindi wa Boris Johnson “ni habari mbaya kwa Ulaya.”

“Ameshinda na sasa kwa bahati mbaya watatoka” alisema Waziri Mkuu Andrej Babis.

Mwenyekiti wa Baraza la Ulaya, Charles Michel amempongeza Johnson na kusema Ulaya iko tayari kujadiliana kuhusu makubaliano ya biashara huru lakini amekwepa kusema kama makubaliano hayo yanaweza kufikiwa katika kipindi cha mwaka mmoja.

DW

# Mwisho wa kutoa kaboni Ulaya sasa mwaka 2050

**BRUSSELS,** Ubelgiji

VIONGOZI wa Umoja wa Ulaya (EU) wamekubaliana kanda hiyo kukomesha utoaji wa gesi ya ukaa au kaboni ifikapo mwaka 2050, katika makubaliano ambayo hata hivyo yalitiwa kiwingu na uamuzi wa Poland wa kukataa kutekeleza lengo hilo.

Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, alisema makubaliano yaliyoafikiwa jana wakati wa mkutano wa wakuu wa nchi wa EU jijini Brussels, ni uthibitisho madhubuti unaoiweka Ulaya katika mstari wa mbele kwenye juhudi za dunia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Michel alisema makubaliano yaliyofikiwa ni muhimu kwa Ulaya kuonyesha nia yake linapokuja suala la kupambana na uchafuzi wa mazingira.

Kwa upande wake Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen ameyasifu makubaliano yaliyofikiwa baada ya majadiliano makali yaliyojumuisha wasiwasi kuhusu uwezekano wa kufikiwa malengo yaliyopendekezwa.

“Tumenuwia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuyageuza kuwa fursa kwa Umoja wa Ulaya, tukifahamu kuwa sasa EU ndiyo kinara kwenye suala hilo na tunataka kuendelea kuwa kinara, kuwa mfano wa kuigwa,” alisema Von der Layen jijini Brussels. Makubaliano hayo yalitiwa doa na uamuzi wa Poland nchi mwananchama wa Umoja wa Ulaya inayotegemea kwa sehemu kubwa nishati ya makaa ya mawe, kusema haiko tayari kusitisha haraka matumizi ya nishati chafuzi ifikapo mwaka 2050.

Kulingana na wanadiplomasia mjini Brussels, Poland inahitaji pengine hadi mwaka 2070 ili kuhamia kikamilifu katika kutumia nishati rafiki kwa mazingira, huku mataifa mengine kama jamhuri ya Czech yakipigia upatu kuendelea kutumiwa nishati ya nyuklia.

Ili kujizuia na aibu ya kuanguka kwa makubaliano yaliyofikiwa kutokana na upinzani wa Poland, viongozi wa Umoja wa Ulaya wameidhinisha kipengele mahsusi kitakachowezesha hoja za Poland kujadiliwa kwa upana wakati wa mkutano mwingine wa kilele mwezi Juni mwaka 2020.

Makubaliano ya mjini Brussels ni matokeo ya mpango wa kufikia Ulaya isiyochafua mazingira ambao ulizinduliwa Jumatano iliyopita.

Mpango unajumuisha kukusanya Euro bilioni 100 kuzisaidia nchi wanachama kuhamia katika matumizi ya nishati jadidifu.

DW

# HADITHI

## JUMBA JEKUNDU-31

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

==================================================




"Ila nina ombi moja."

"Omba tu."

"Haya yote siwezi kufanya peke yangu bila ya kuwa na mtu wa kunisaidia, hivyo naomba msaada wako ili tusaidiane. Unajua kuna maeneo nikienda mimi kama mwanamke inakuwa kero kidogo, lakini kama kukiwa na mwanamume kunakuwa na unafuu."

"Siwezi kukupinga hata kidogo Edina, umefanya mambo mengi juu yangu na mimi sasa ni wakati mzuri wa kuonyesha mrejesho wa kile ulichonitendea kuulinda uhai wangu."

"Usijali Kadili wewe ni rafiki yangu, swahiba yangu, nimeutetea uhai wako kwa gharama zote kwa sababu wewe kwangu ni mtu muhimu mno."

"Ndiyo maana nikasema kuwa nitafanya chochote kile, hata kama ukitaka nisimame juu ya bahari. Kwa sababu hapa nitakachofanya ni kulipa tu wema ulionifanyia ambao utakuwa ni wa kuiga tu. Wewe wa kwako Edina ni wa asili kwa sababu ulianza mwanzo bila kutegemea malipo au wema kutoka kwangu kwa hiyo wema wa asili na wa kuiga hatolingana kamwe."

Maneno hayo yalimchoma Edina, alinyanyuka taratibu na kumfuata Kadili. akamkumbatia. Ilionekana kabisa hawa wote wawili wana kitu ndani ya mioyo yao ambayo hawataki kuweka wazi.

Kadili ndani ya moyo wake alikuwa anampenda Edina, lakini ufukara na woga ndiyo uliomfanya ashindwe kabisa kumwambia neno 'Nakupenda'. Tangu alipokutana naye kwa mara ya kwanza 'blue star' kule Sinza hadi muda huo anakumbatiwa na mtoto huyo mkali wa kitajiri, mwenye uzuri usiomithilika, Kadili alikuwa akifa na kidonda cha roho.

Pamoja na wema wote aliomtendea na kuonekana kumjali hadi muda huo, Kadili bado alikuwa hajui ndani ya moyo wa Edina alikuwa akifikiria nini. Alifanya hivyo kwa sababu tu ya kumuonea huruma kutokana na matatizo yote aliyasababisha yeye, au Edina alikuwa na lake moyoni?

**Siwezi kukupinga hata kidogo Edina, umefanya mambo mengi juu yangu na mimi sasa ni wakati mzuri wa kuonyesha mrejesho wa kile ulichonitendea kuulinda uhai wangu.**

***********************************

Akili yake ya kwaida tu Eliza alijua kuwa Kadili hampendi kwa dhati. Labda amelazimishwa tu na mama yake.

Baba yake mzazi na mama yake Kadili wanataka waoane kwa sababu zao binafsi. Eliza, msichana wa haja, si kwamba hakuwa na mpenzi. Ila alichotaka sasa ni mwanaume wa kumuoa. Hakutaka kuhangaika na kuharibia heshima wazazi wake. Ndiyo maana baba yake alipomfuata na kumwambia aolewe na binamu yake Kadili hakupinga.

Kwa sasa ametoka kwao Mtoni Mtongani na kuishi Tandale kwa sababu tu ya kuwa na ukaribu na Kadili.

Hata hivyo, mwenzake hakuonekana kumjali sana na wala hakuonekana kumkataa.

Penzi huonekana zaidi kuliko kusikika, Eliza alijua kabisa kuwa Kadili kuna mtu ana mpenda. Naye ni Edina.

Hata hivyo kuna stori nyingi anazozisikia za msichana huyo kuwa ametoka kwenye familia ya kitajiri, hali inayomsababishia matatizo binamu yake. Vinginevyo saa hizi wangeshakuwa mke na mume.

Kuolewa na mtu ambaye ndani ya moyo wake kuna mtu mwingine anampenda, ila tu kwa sababu kuna vipingamizi, ilimuwita tabu kidogo.

Tayari alikuwa ameshafika dukani kwa Meze, rafiki ya Kadili. Kuna kitu alikwenda kununua, lakini pia kumuangalia kama Kadili huko huko, kwani ni muda mrefu umepita.

"Kadili hata mimi sijamuona muda mrefu sasa." Alijibu Meze na kuongeza.

"Mimi nilidhani uko naye nyumbani huko."

"Hapana aliondoka muda mrefu sana, mpaka saa hizi inafika saa tatu usiku bado hajaonekana."

"Eliza wacha wivu, mumeo mtarajiwa atarudi tu, au unadhani yuko na wanawake wengine?' Alihoji.

"Mhh, hapana usalama wake muhimu kwanza."

"Siyo wivu bibie?"

"Hapana sina wivu kwa sababu sidhani kama rafiki yako ananipenda hasa."

"Kwa nini?"

"Huo unafiki, hata wewe unajua hilo. Kuna mtu anampenda, ndiyo anayemsumbua, na mimi nimekuwa kama mbadala tu, ikishindikana kabisa ndiyo anioe mimi."

"Sasa hilo linakukwaza?"

"Sana tu, nimekubali kwa sababu wanaotaka hili litimie ni shangazi yangu, mama yake Kadili na baba yangu mzazi mzee Tengeneza, kaka yake shangazi, vinginenvyo nisingekubali."

"Ila kuolewa unataka?"

"Meze, hakuna mwanamke asiyekubali kuolewa. Lakini anataka kuolewa na mwanaume anayempenda na kumjali, lakini kwangu mimi kwa Kadili ni kama spea tairi ambalo linasubiri lingine liharibike, ndiyo litumike, kama halikuharibika ndiyo basi tena."

Meze alimuangalia kwa makini Eliza. Aligundua uzuri usio na shaka aliokuwa nao. Ni kwa sababu tu tayari ndani ya ubongo wa Kadili kuna picha ya Edina, vinginevyo msichana huyu alifaa kuolewa.

"Kama mimi nigekuwa Kadili, saa hizi ningekuwa nimeshakuoa." Maneno hayo yalimtoka Meze bila kutarajia.

"Inawezekana wewe unajua thamani yangu na si rafiki yako."

"Hakika, Eliza wewe ni mwanamke mrembo, mwenye kila sifa ya kuwa malkia ndani ya nyumba. Bahati hii haikunikuta mimi, nisingeipoteza."

"Haijakukuta kwa sasa, lakini huenda baadaye ikakukuta." Alijibu Eliza huku akiondoka taratibu kwa madaha na kumuacha Meze na maswali mengi na kitu moyoni.

Kwa mbali alionekana kuvutiwa na Eliza. Tatizo lilikuwa ni rafiki yake Kadili. Pia isingewezekana kwa sababu wazazi wa Kadili na msichana huo ambao ni ndugu, tayari akili yao ilikuwa ni kuwaozesha vijana hao.

Kwa upande wa Eliza alionekana kufarijika na maneno matamu kutoka kwa Meze ambayo hajawahi kuambiwa hata siku moja na mumewe mtarajiwa Kadili.

"Nikipata mume kama yule si nitaringa." Alijisemea mwenyewe.

***********************************

Kama kawaida yake, ukiona mama Gombea anapitapita kwenye nyumba za jirani zake ujue kuwa kitu.

Anapeleka umbea, au anatembeza sare za ngoma.

"Mama Kadili habari za asubuhi?" Alisalimia akiwa nje, baada ya kutomuona mtu yoyote ndani.

"Nzuri tu, mbona asubuhi asubuhi mama Gombea kwema huko, maana wewe mwenzangu, una mambo wewe."

"Aka mwenzangu nimepita tu kukusalimia, nakwenda kudai madeni yangu, maana kuna wengine lazima uende saa hizi, maana ikishafika saa tatu au nne, hukuti, wameshakimbia majumba yako, chezea madeni wee."

"Hebu toka kidogo shosti nakuhitaji."

Mama kadili alijua kabisa kuna ubuyu. Kwa sababu mama Gombea anajulikana sana mtaani kwa kazi hiyo.

Hakuna ambacho kinampita. Hakuna ambacho hakifahamu.

"Huyo mwanao Kadili yupo?" Mama Gombea aliuliza baada ya mwezake kutoka nje.

"Amelala."

"Na huyo mchumba wake mtarajiwa?"

"Ametoka kwenda kuwasaidia mawifi zake kuuza supu barabarani."

"Shoga jana kwa macho yangu haya mawili, nimewaona."

"Nani mama Gombea, mbona unanitisha?"

"Huyo mwanao binti ya kaka yako."

"Eliza?"

"Nani mwingine. Huyo huyo, pamoja na Meze. Nimewaona usiku pale dukani. Nimekuja kukwambia shoga kuwa kumbe Meze anamzunguka mwenzake, anatembea na Eliza. Kwa macho yangu haya mawili nimeshuhudia."

**Itaendelea Jumamosi**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KAZI /AJIRA**

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**

**PROSHARE CAPITAL LTD**

Kutangaza magari yanayouzwa;

- BRIAN F. LYARUU (TOYOTA ALTEZZA T 297 BLC)
- HALIFE S. HALIFE (MITSUBISH FUSO T 559 CZG
- MRISHO M. JUMA (HONDA T 598 BVM)
- JONATHAN Z. MHANDO (MITSUBISHI CANTER T 105 BCV)
- JANETH P. BOAZ (TOYOTA IST T 120 DQE)
- JIMMY R. TILLYA (T/SPRINTER T 500 BJM)

115555302

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili MC 452 AXF, Chassis No. MD2A21BZ3FWE75046, Engine No.PFZWFE56923.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/514946/2019.

215555602

**KADI YA GARI IMEPOTEA**

INNOCENT MICHAEL NDANGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA KLUGER yenye namba za usajili T 188 DRV. Chassis No. ACU20003l530. Engine No. 2AZ0669919. Yenye rangi NYEUSI. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.

Taarifa ya Polisi: MWA/IGO/RB/520/426/2019.

215555702

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**JEREMIA NYAMPALA SHILLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili T 457 CNN aina ya SUNLG.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/JNIA/546767/2019.

115555802

**KUPOTEA KWA KADI**

Gabriel Mbwambo Irigo anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T427 AZJ iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania, gari aina ya PREMO.

Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/KIJ/RB/537954/2019

215555202

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# Sarri amtaka Mourinho mtoano 16-bora Uefa




**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, angependa kukutana na Tottenham Hotspurs katika hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ili aweze kukutana na "asiyetabirika" Jose Mourinho.

Mabingwa hao wa Italia walitinga kiurahisi kwenye hatua hiyo ya mtoano baada ya ushindi mara tano na sare moja kwenye Kundi D, wakishindi 2-0 dhidi ya Bayer Leverkusen, Jumatano.

Tottenham ilikumbana na kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Bayern Munich kwenye mchezo wake wa mwisho wa Kundi B, ingawa walikuwa tayari wana uhakika wa kumaliza nafasi ya pili dhidi ya miamba hao wa Kundi B.

Juve na Tottenham wanaweza kukutana kwenye raundi ijayo, huku Chelsea, Borussia Dortmund, Lyon na Real Madrid pia wakiwa na uwezekano wa kukutana na Juventus.

Mourinho alidai kwamba, timu zitakuwa zinaogopa kukutana na Tottenham, lakini Sarri yeye yupo wazi kutaka kukutana na kocha huyo raia wa Ureno, ambaye awali walikutana kwenye Ligi Kuu ya England.

"Nina heshima ya kumjua Mourinho," alisema kocha huyo wa zamani wa Chelsea.

"Yeye ni mtu asiyetabirika kwamba yupo tofauti kabisa na mtazamo wa dunia ulivyo.

"Ilikuwa ni kitu cha kufurahisha kumjua yeye. Kucheza dhidi yake sio kazi rahisi, lakini kumuona nikicheza naye ni jambo kubwa."

Juventus itaingia kwenye droo ya Jumatano na vinara wenzake wa makundi kama Paris Saint-Germain, Bayern Munich, Manchester City, Liverpool, Barcelona, RB Leipzig na Valencia.

Alipoulizwa kama ana nafasi kubwa ya kwenda kulibeba taji hilo, Sarri alijibu: "Manchester City."

Juventus inarudi kwenye Serie A Jumapili ikikabiliwa na mchezo wa nyumbani dhidi ya Udinese.

# Fedha tatizo Ancelotti kutua Everton, Arsenal



**NAPLES**, Italia

WAKATI klabu za Arsenal na Everton zikitajwa kuwania kumchukua kocha Carlo Ancelotti, lakini kiwango cha fedha kinaweza kuwa kikwazo, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu hizo mbili zinahusishwa na kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Ancelotti baada ya kufukuzwa kule Napoli katikati ya wiki.

Mtaliano huyo anatajwa kuwa na nafasi kubwa ya kutua pale Arsenal kwenda kuchukua mikoba ya Unai Emery licha ya kudaiwa kwamba kuna orodha ya makocha wasiopungua 10 wanaohusishwa na klabu hiyo ya Emirates.

Everton pia nao wanamtaka baada ya kumfuta kazi Marco Silva wiki iliyopita.

Lakini, taarifa zinadai kwamba Ancelotti anaweza kuwagharimu fedha nyingi timu hizo.

Kinachoelezwa ni kwamba Ancelotti bado yupo kwenye mambo ya kumalizia kuhusu kuachana na Napoli na hapo atafahamu kama ameachwa jumla au bado anabaki kwenye ratiba ya mishahara ya Napoli hadi mkataba wake utakapofikia tamati.

Napoli ilifanya hivyo ilipoachana na Maurizio Sarri kipindi ambacho ilimchukua Ancelotti.

Napoli kwa sasa itakuwa chini ya mchezaji wa zamani wa Ancelotti, Gennaro Gattuso, aliyewahi kumnoa huko AC Milan.

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Fenerbahce ya Uturuki, Vedat Muriqi, ameripotiwa kuwaniwa na klabu za Manchester United na Tottenham Hotspurs.

Mshambuliaji huyu mwenye mabao 10 katika mechi 14 amekuwa akimvutia kocha wa Tottenham, Jose Mourinho.

Gazeti la Per Milliyet la Uturuki limeripoti kwamba, mchezaji huyo mwenye miaka 25, amekuwa akitafutwa mara kwa mara na Spurs.

Nyota huyo wa kimataifa wa Albania pia amefunga mabao 23 mojawapo ni bao alilofunga katika mchezo wao wa hivi karibuni dhidi ya England ambapo walichapwa 5-3.

Muriqi pia anawindwa na klabu ya Bournemouth na kinachosubiriwa ni klabu yake kupokea ofa kutoka klabu mojawapo.




# United, Spurs zaingia vitani

# Solskjaer: Greenwood na Rooney? Hapana



**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer ameweka mbali kumfananisha kati ya Mason Greenwood na Wayne Rooney baada ya mshambuliaji huyo kinda kung'ara wakati Manchester United wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya AZ.

United iliendelea kuwa na Desemba nzuri licha ya kuwa na mwazo mgumu kipindi cha kwanza dhidi ya wapinzani wao hao kutoka Ligi Kuu ya Uholanzi 'Eredivisie', huku Greenwood akitamba.

Baada ya Ashley Young kufunga bao la ufunguzi, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alifunga mara mbili na kupata penalti moja iliyofungwa na Juan Mata.

Mabao yote yalifungwa ndani ya dakika 11 ya kipindi cha kwanza, na sasa vijana hao wa Solskjaer wakisubiri droo itakayopangwa Jumatatu katika hatua ya mtoano.

"Ni mmaliziaji wa daraja tofauti," alisema Solskjaer akiiambia BT Sport. "Ndani na nje ya bosi unatarajia yeye kupiga shuti. Yupo vizuri kwenye umaliziaji.

"Yupo vizuri kwenye kujitengenezea nafasi yeye mwenyewe."

Solskjaer aliulizwa kama anamlinganisha mchezaji huyo na Rooney ambaye alianza mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akiwa na umri wa miaka 18 na akafunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Fenerbahce.

"Hapana, hapana, hapana. Yeye ni mchezaji tofauti kabisa, Mason ni tofauti na Wazza, lakini lazima afurahie usiku wake," alisema.



# Carvajal amtaka Mbappe ajiunge Real Madrid

**MADRID,** Hispania

DANI Carvajal angependa Kylian Mbappe aondoke Paris Saint-Germain kwenda Real Madrid wakati anaamini wachezaji bora duniani wanatakiwa kuwa katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Nyota huyo wa Ufaransa, Mbappe ameendelea kuhusishwa kuhamia Madrid na imeripotiwa kwamba mazungumzo kuhusu mkataba mpya na PSG yamesimama.

Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane ameonyesha mara kadhaa kuvutiwa kwake na straika huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye uhusiano wake na kocha wa PSG, Thomas Tuchel kwa siku za hivi karibuni umeonyesha ishara ya kutokuwa mzuri, hasa Mbappe alipompoteza wakati alipotolewa nje dhidi ya Montpellier wikiendi iliyopita.

Carvajal angependa kuona Mbappe anahamia kwa miamba hao wa mji mkuu wa Hispania, na aliwaambia waandishi wa habari Alhamisi: "Kile tulichokiona kipo wazi.

"Ni mmoja wa wachezaji wakubwa na itakuwa vizuri kucheza naye kwa sababu vitu bora vinatakiwa kuwa hapa."

Beki wa Madrid, Carvajal alikuwa akizungumzia wiki ngumu kwa Madrid, ambao watawavaa Valencia kwenye dimba la Mestalla kesho, Jumapili kabla ya Jumatano ijayo kuingia kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya Barcelona katika Uwanja wa Camp Nou.

Mchezo huo awali ulitakiwa kupigwa Oktoba, lakini ukaahirishwa kutokana na maandamano ya kisiasa yaliyotokea kule kwenye Jimbo la Catalunya.

# Saka amshitua Ljungberg Arsenal



**LONDON,** England

KOCHA wa muda wa Arsenal, Freddie Ljungberg, ameonyesha kukunwa zaidi na kinda mwenye umri wa miaka 18, Bukayo Saka "kwa kiwango cha kuvutia" wakati akiwaokoa dhidi ya Standard Liege.

Saka alicheza vizuri na kufunga bao la kusawazisha kwa Arsenal wakati wakitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Standard kwenye mchezo wa mwisho wa makundi ya Kombe la Ligi ya Europa, Alhamisi.

Winga huyo kinda pia alitengeneza krosi safi kwa Alexandre Lacazette kufunga bao wakati vijana hao wa Ljungberg wakiwa nyuma kwa mabao 2-0.

Ushindi huo uliwasaidia 'Washika Bunduki' hao kupata pointi kwenye mchezo huo wa Kundi F, mbele ya Eintracht Frankfurt wanaowafuatia.

"Alinivutia," alisema Ljungberg akimzungumzia Saka baada ya mchezo huo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Mpira wake wa mwisho, ulikuwa na maana kubwa na alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi.


"Mwanzo kabla ya mchezo kwa kiasi fulani alionekana kutofurahishwa na uamuzi wa kuchezeshwa winga ya pembeni. Ana kipaji cha ajabu.

"Nawaonea huruma wachezaji wangu vijana. Wengi wao hawajapelekwa kucheza kwa mkopo, hawana uzoefu wa kutosha kwa timu kubwa.

"Baadhi yao wanafanya makosa, lakini wanajifunza kutokana na makosa hayo na huwa wanayarudia wakati mwingine. Lakini Bukayo alionyesha kipaji cha ajabu."

Arsenal kwenye mchezo huo iliwatumia zaidi wachezaji vijana hasa kwenye safu ya ulinzi na Ljungberg alionekana kuwa na imani nao dhidi ya Standard.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AITAMANI MADRID FAINALI UEFA

●●● Real ni timu ya kipekee, lakini kama utaniuliza mimi, ningependa zaidi kukutana nayo baadaye...

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo, anatumai kukutana na klabu yake ya zamani ya Real Madrid katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Ronaldo aliifungia Juventus katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Bayer Leverkusen Jumatano wakati wakimaliza mechi zao za Kundi D kwa kushinda michezo mitano na sare moja.

Mabingwa hao wa Italia wataungana katika hatua ya mtoano na vinara wa Kundi A, Real Madrid, klabu ambayo Ronaldo ana kumbukumbu ya kuitumikia kwa miaka tisa kabla ya kutimkia hapo Turin mwaka jana.

Real Madrid ni miongoni mwa timu tano ambazo Juve inaweza kukutana nazo katika hatua ya 16-bora, sambamba na Chelsea, Borussia Dortmund, Lyon na Tottenham, lakini Ronaldo anatumai kuwakwepa miamba hao wa LaLiga kwa sasa.

**“Real ni timu ya kipekee, lakini kama utaniuliza mimi, ningependa zaidi kukutana nayo baadaye,” Ronaldo, ambaye alitwaa ubingwa wa Ulaya mara nne akiwa na Madrid, aliiambia Sky Sport Italia.**

“Katika fainali? Ningesaini sasa kukutana nao fainali.”

Ronaldo amefunga katika mechi tatu mfululizo za Juventus na kujisikia kuwa vizuri kabisa kutokana na jeraha lililompunguzia nafasi ya kucheza mwezi uliopita.

“Ninajisikia vizuri, matatizo ya kiutimamu wa mwili niliyopitia,” alisema. “Ilikuwa ni wiki nne nilizocheza na maumivu kidogo, lakini sasa nipo vizuri.

“Timu inafanya vizuri. Tulicheza vizuri katika kipindi cha pili [dhidi ya Leverkusen] na tumekuwa wa kwanza katika kundi letu. Mambo yameimarika kwangu pia, ninajiamini zaidi na ninatumai kuendelea kama hivi.”

Maurizio Sarri alidai wiki iliyopita kuwa haiwezekani kumtumia Ronaldo, Paulo Dybala na Gonzalo Higuain kwa pamoja katika safu ya ushambuliaji, na badala yake kocha huyo wa Juventus alikuwa akipendelea zaidi kuwachezesha kwa zamu.

Ronaldo amekiri kuwa anapenda zaidi kucheza na washambuliaji hao wawili wa Argentina lakini ni mwenye furaha kufuata mpango wa Sarri.

“Ikiwa ninacheza na Dybala ama Higuain, ni vizuri,” alisema.

“Ninapenda kucheza nao wote, tuna furaha sana uwanjani, lakini kocha ndiye anayepaswa kufanya uamuzi na lazima tuuheshimu.

“Lakini siwezi kukataa kwamba tunafurahia sana.”

## KWA UFUPI

### UNITED YAJIAMINI KWA SANCHO
MANCHESTER United inajiamini itafanikiwa kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Muingereza Jadon Sancho, 19, mwezi ujao na pia inaweza kumfuata kiungo wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27. (Mirror)

### GUARDIOLA ANUKIA KUSEPA CITY
PEP Guardiola amevunja kipengele chake kinachomtaka kuununua mkataba wake, jambo ambalo linaweza kushuhudiwa akiondoka Manchester City mwishoni mwa msimu huu. (Mail)

### POCHETTINO AWINDWA WEST HAM
WEST Ham ina malengo ya kumteua kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino ili kurithi mikoba ya Manuel Pellegrini. (Star)

### ANCELOTTI KIRAHISI ARSENAL
ARSENAL na Everton hazitahitajika kuilipa Napoli fidia yoyote kama zitamteua Carlo Ancelotti, ambaye alitimuliwa na miamba hiyo ya Italia mapema wiki hii, kuwa kocha wao. (Mail)

### EVERTON WATETA NA EMERY
EVERTON imefanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Arsenal, Unai Emery lakini hawezi kumteua Mhispania huyo, ambaye yupo tayari kufanya kazi tena Ligi Kuu England. (ESPN)

### HAALAND KUTETA NA UNITED, JUVE
MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg na mzaliwa wa Leeds, Mnorway Erling Braut Haaland, 19, anapendelea kupata ofa kutoka kwa Borussia Dortmund na RB Leipzig, lakini anatarajiwa kufanya mazungumzo na Manchester United pamoja na Juventus kabla ya kuamua kuhusu mustakabali wake wa baadaye. (Guardian)

### ZAHA KUIGHARIMU CHELSEA
CRYSTAL Palace itahitaji pauni milioni 80 ili kumwachia mshambuliaji wa kimataifa wa Ivory, Wilfried Zaha, 27, ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea. (Evening Standard)

### NAPOLI KUMPANDIA DAU TORREIRA
NAPOLI inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 21 kwa kiungo wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira kama haitamruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kuondoka kwa mkopo katika dirisha dogo la usajili la Januari. (Il Mattino - in Italian)

### NEYMAR AFURAHIA MAISHA PSG
MSHAMBULIAJI Mbrazil Neymar, 27, ameahidi ni mwenye “furaha” hapo Paris St-Germain, mchezaji huyo alitaka kuondoka Ufaransa mapema msimu huu. (AS)

### PEDRO AITAKA TENA BARCA
WINGA wa Chelsea, Mhispania Pedro Rodriguez, 32, ambaye atamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu, angependa kukaribisha nafasi ya kucheza tena Barcelona. (Sport)

### ROSE AMFUNGUKIA MOURINHO
BEKI Muingereza Danny Rose, 29, amesema hahitaji kujadili mustakabali wake wa baadaye na kocha wa Tottenham, Jose Mourinho na kwamba bado atahitaji kumaliza mkataba wake. (Mirror)

### REDKNAPP ATAJWA WEST HAM
KOCHA wa zamani wa West Ham, Harry Redknapp pia ameibuka kama mmoja wa makocha wanaotarajiwa kuteuliwa tena kuwanoa ‘Hammers’ hao. (Football Insider)

# MGUNDA: NI KUFA KUPONA TUKIIVAA SUDAN CECAFA LEO

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

MBIVU mbichi kuhusu hatima ya timu ya Tanzania Bara "Kilimanjaro Stars" kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la Chalenji itajulikana katika mechi yake ya mwisho ya Kundi B dhidi ya Sudan itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KCCA jijini hapa.

Kilimanjaro Stars yenye pointi nne itashuka dimbani katika mechi ya leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0, walioupata baada ya kuwafunga "ndugu zao" Zanzibar (Zanzibar Heroes), katika mchezo uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Stars, Juma Mgunda, alisema mechi ya leo itakuwa ngumu, lakini wataingia kwa tahadhari huku wakiwaheshimu zaidi wapinzani wao Sudan.

Mgunda alisema kuwa mechi ya leo ni zaidi ya fainali na wataingia uwanjani kwa ajili ya "kucheza kufa au kupona" kwa sababu wanataka kusonga mbele kwenye mashindano hayo.

"Tunatarajia kuwa na mchezo mgumu na wenye ushindani, hatutawadharau wapinzani wetu kwa sababu nao pia wana nafasi ya kusonga mbele, utakuwa ni mchezo wenye ushindani kutokana na kila upande kujipanga kusaka matokeo chanya," alisema Mgunda.

Naye Kocha Mkuu wa Sudan, Mohammed Mussa Dawoud, alisema hawajakata tamaa ya kusonga mbele katika mashindano hayo na leo wataingia na mipango tofauti.

"Tulifungwa mchezo uliopita, lakini bado tuna nafasi na hakuna lisilowezekana, tuna uwezo wa kushinda katika mechi yetu ya mwisho dhidi ya Tanzania na kutinga hatua ya nusu fainali, tumejipanga kucheza soka la kiwango cha juu ili tutimize malengo," alisema Dawoud.

Alisema wachezaji wake wote wako tayari kwa mechi hiyo ambayo ni muhimu katika kampeni ya kuwania ubingwa wa michuano ya mwaka huu.

Mechi nyingine ya Kundi A itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Zanzibar Heroes dhidi ya mabingwa watetezi Kenya (Harambee Stars) wakati Kundi B wenyewe watamaliza michezo yao kesho Jumapili kwa Somalia kuivaa Burundi wakati Uganda ambao tayari wameshatinga hatua ya nusu fainali wakivaana na Djibouti.

## MKESHA...



Mwimbaji wa nyimbo za Injili, Sarah Mwangi, maarufu Sarah K, kutoka Kenya, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkesha wa maombi utakaofanyika kwenye viwanja vya Tanganyika Packers Kawe, ukiambatana na uimbaji utakaoshirikisha waimbaji mbalimbali wa hapa nchini. Wengine kutoka kulia ni washiriki wa tamasha hilo, Gwamaka Mwakibete, Paul Mwangosi na Jeremy Kitiku (kusoto). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasichana Bara U-17 walipa kisasi vipigo Kenya

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

BAADA ya dada zao kufungwa na Kenya katika fainali za Kombe la Chalenji mwezi uliopita huku pia kaka zao wakichapwa tena na Harambee Stars kwenye michuano hiyo inayoendea nchini hapa, timu ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara wamewafunga wenzao wa Kenya mabao 3-1 katika mechi ya michuano hiyo ya vijana iliyochezwa kwenye Uwanja wa Njeru mjini hapa jana.

Kwa matokeo hayo, Tanzania Bara sasa imefikisha pointi saba na kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa kwanza wa mashindano hayo yanayoshirikisha timu za Afrika Mashariki na Kati.

Hadi mapumziko, wasichana hao wa Tanzania Bara walikuwa mbele kwa mabao 2-1, hali iliyowafanya kipindi cha pili warejee wakiwa na kasi ya kupambana kupenya ngome ya Kenya ambayo ilicheza zaidi kwa kujilinda.

Mabao ya Tanzania Bara katika mchezo huo yalifungwa na Thabea Munga, Joyce Meshack kwa penalti na Aisha Masaka wakati Fasila Adhiambo alifunga goli pekee la Kenya.

Hata hivyo, Tanzania Bara inahitaji kuwafunga wenyeji Uganda katika mechi itakayochezwa kesho saa 10:00 jioni ili kukaribia kutwaa kombe hilo wakati mechi yao ya mwisho itachezwa Jumanne dhidi ya vibonde Djibouti.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Bara, Edna Lema, amewapongeza wachezaji hao kwa kiwango kizuri walichokionyesha na kusema kwamba wanahitaji utulivu zaidi katika mechi inayofuata ili kujihakikishia ubingwa.

"Mashindano haya ni magumu, lakini kikubwa wachezaji wetu wameanza kuelewa kile tunachokitafuta, naamini wakitulia zaidi na kufuata maelekezo tuliyowapa, tutafanya vizuri pia, ushindi wa leo (jana), utarejesha hamasa tuliyoizoea," alisema Edna.

Katika mechi ya mapema jana asubuhi, Burundi ilipata ushindi wa kwanza kwa kuwafunga Djibouti mabao 8-0 na hivyo kufikisha pointi nne.

# Simba Queens, Yanga Princess zaidi ya vita leo

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI Kuu ya Wanawake raundi ya nne inaendelea leo ambapo timu ya Yanga Princess itakuwa na nafasi ya kulipa kisasi dhidi ya Simba Queens, zitakapokutana leo katika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam katika mchezo ambao mashabiki wataushuhudia bure bila kiingilio.

Msimu uliopita Simba Queens ilishinda mechi zote mbili ambapo katika mzunguko wa kwanza iliichapa 7-0 kabla ya raundi ya pili kuikung'uta 5-1.

Alizungumzia mchezo huo jana, Ofisa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto alisema wameamua kutoweka viingilio katika mchezo huo kwa lengo la kuzidi kuinua soka la wanawake.

"Sisi kama TFF tutahakikisha ulinzi unakuwa wa kutosha kwenye mchezo huo, tunaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kushuhudia mtanange huo," alisema Kizuguto.

Alisema wameamua kutumia Uwanja wa Karume kutokana na kuombwa na wenyeji wa mchezo huo, ambao ni Yanga.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Nassoro Muhusini, alisema wamejipanga vizuri kwa ajili ya kukutana na Simba Queens wakati na kwamba hadi sasa hana majeruhi hata mmoja.

"Nimekiandaa vizuri kikosi changu lengo ni kuibuka na ushindi mnene kesho( leo) tunaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi,"alisema Nassoro.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Mgosi alisema licha ya Yanga kusajili wachezaji wazuri hauhofii mchezo huo na badala yake anahitaji pointi tatu.

"Tutaingia kwa tahadhari kubwa uwanjani kwa sababu ninaiheshimu Yanga ina wachezaji wazuri tofauti na waliokuwapo msimu uliopita lengo ni kufanya mapinduzi ya soka la wanawake," alisema Mgosi.

# Mwenyekiti Stand United ajiuzulu

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

MWENYEKITI wa timu ya Stand United ya mkoani Shinyanga, Dk. Herison Maeja, ametangaza kujiuzulu nafasi hiyo, kwa kile alichokieleza kuwa ni kuzidiwa na majukumu ya kazi zake binafsi.

Maeja ametangaza nia yake kujiuzulu katika nafasi hiyo jana, wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, kuwa ifikapo Desemba 15, mwaka huu, hatakuwa tena Mwenyekiti wa Stand United.

"Kutokana na kuzidiwa na majukumu ya kazi zangu, sitakuwa na nafasi ya kuweza kutekeleza majukumu magumu na mazito ya klabu kwa ufanisi, hivyo kwa heshima na taadhima ninaomba kujiuzulu nafasi ya uenyekiti wa klabu ya Stand United FC ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

"Kwa unyenyekevu mkubwa shukrani zituendee sisi sote pale timu yetu ilipofanya vizuri na kuleta sifa kwa Wanashinyanga kwa kushirikiana na viongozi wenzangu, wanachama, wapenzi, na wadau mbalimbali, jina la Mungu lipewe sifa, lakini pale ambapo timu haikufanya vizuri changamoto kubwa ilikuwa ni ukosefu wa fedha," alisema Maeja ambaye alijiunga na Stand United kama mwanachama wa kawaida mwaka 2013 kabla ya kuukwaa uwenyekiti miaka mitatu baadaye.

# Michezo

Jumamosi Desemba 14, 2019

Nipashe


Ronaldo aitamani Madrid fainali Uefa



HABARI UK. 30

# Dante, Tariq wakinogesha kikosi Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

YANGA imeanza kunoga 'mdogomdogo' baada ya kujiimarisha kwa kumsajili mshambuliaji chipukizi Mtanzania Tariq Seif, aliyejiunga na klabu hiyo akitokea nchini Misri alipokuwa anacheza soka la kulipwa huku ikifanikiwa kumrejesha kikosini beki wao kisiki, Andrew Vincent 'Dante'.

Tariq aliyekuwa anachezea klabu ya Dekernes FC ya Daraja la Pili nchini Misri ambayo alijiunga nayo msimu huu akitokea Biashara United ya Mara, aliwasili juzi jijini Dar es Salaam na kupokewa na Katibu Mkuu wa Yanga, David Ruhago kabla ya jana Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla kumtambulisha rasmi kupitia ukurasa wa Instagram wa klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo, Tariq ambaye msimu uliopita aliitungua Yanga katika mechi ya Ligi Kuu wakati akiichezea Biashara United, anaelezwa kulazimika kurejea nchini ili kunusuru kiwango chake kutokana na kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza cha Dekernes FC.

Kabla ya kutua Biashara United, Tariq anayetarajiwa kuwa pacha wa David Molinga dimbani baada ya Mnamibia Sadney Urikhob na Mganda Juma Balinya kuachana na klabu hiyo, alianzia soka lake katika Klabu ya Transcamp kisha Mbao FC.

Katika hatua nyingine, kurejea kwa Dante katika kikosi cha Yanga kumetokana na klabu hiyo kushinda rufaa dhidi ya beki huyo baada ya kukata rufaa Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Yanga walimkatia mchezaji huyo rufaa hiyo TFF baada ya Dante kugoma kurejea kikosini akishinikiza alipwe kwanza stahiki zake mbalimbali, ikiwamo fedha za usajili.

Na jana uongozi wa Yanga, ulisema: "Uongozi wa mabingwa wa kihistoria Tanzania, (Yanga SC) unamkaribisha tena kikosini beki @vicentandrew 'Dante' baada ya kumalizika kwa shauri la kesi baina ya pande mbili."

MWAGA WINO...



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Tariq Seif, akitia saini mkataba wa kujiunga na timu hiyo jana, makao makuu ya klabu hiyo, Jangwani jijini Dar es Salaam mbele ya Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kulia) na Katibu Mkuu, David Luhago. . **MPIGAPICHA WETU**

# SVEN AISHIKA SIMBA MSHIPA WA FAHAMU

●●● Amwaga mikakati mizito ya CAF, aomba siku 10 akieleza mashabiki walivyomvutia na ukijana wake utakavyosaidia..

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Simba, Sven Ludwig Vandenbroeck, licha ya kuomba siku 10 ili kukaa kwanza na timu hiyo kabla ya kuzungumza rasmi na vyombo vya habari nchini, amegusia kitu ambacho ni wazi atakuwa ameugusa 'mshipa wa fahamu' wa uongozi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Baada ya kumtambulisha Jumatano usiku, uongozi wa klabu hiyo ulitangaza kuwa jana kocha huyo angezungumza na waandishi wa habari, lakini baada ya wanahabari kuwasili eneo la tukio wakatangaziwa kuwa mkutano huo umeahirishwa na kwamba Sven ameomba apewe siku 10 za kukaa na wachezaji wake kabla ya kuzungumza na vyombo vya habari.

**Hata hivyo, mashabiki wengi na wadau wa soka baada ya kocha huyo mwenye umri wa miaka 40, kutambulishwa Jumatano wiki hii, kupitia vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii waliponda umri na mafanikio yake wakidai hataweza kuisaidia Simba kufikia malengo yake.**

Kauli hiyo imeonekana kama imemfikia Sven, ambapo jana alikiri yeye ni kijana na kudai ataifundisha timu hiyo kisasa na baada ya muda mfupi wachezaji watakuwa wameshauzoea ufundishaji wake.

"Naomba nipewe muda kama wa siku kumi ndio nitaweza kuweka hadharani mikakati yangu kwa sababu bado sijakaa muda mrefu na timu, nikikaa nao ndio nitajua nini cha kuzungumza," alisema.

Hata hivyo, kupitia ukurasa rasmi wa Instagram wa klabu hiyo, kocha huyo alifunguka kwa kugusia jambo ambalo ni kama ameushika mshipa wa fahamu wa uongozi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo baada ya kueleza sehemu ya mikakati yake ambayo ndiyo kiu kubwa ya klabu hiyo.

"Lengo la kwanza ni kushinda ubingwa wa Ligi Kuu. Nataka kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, nataka kucheza mashindano ya CAF. Nataka Simba iwe kwenye hatua kubwa na kupata matokeo mazuri.

"Kilichonivutia Simba cha kwanza ni wingi wa mashabiki. Ni jambo la kufurahisha kuona mashabiki 60,000 wakikushangilia inakupa hisia za kipekee," Sven alisema.

Sven jana aliendelea kukinoa kikosi hicho katika mazoezi yanayoendea kwenye Uwanja wao wa Simba Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake Kaimu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda alisema: "Kikao kilikuwa kifanywe leo [jana] kocha azungumze na waandishi wa habari, lakini tumeahirisha tutakifanyika siku nyingine itakayopangwa," alisema Kaduguda.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >